# CHAMA CHA MAPINDUZI

# MWONGOZO WA CCM
# 1981

**Kimetolewa na Makao Makuu ya CCM**
**S.L.P. 50, DODOMA.**
**Novemba, 1981**

# YALIYOMO

Ukurasa

**DIBAJI** ………………………………………………………… i

**SEHEMU YA KWANZA**
UTANGULIZI ………………………………………………………… 1-7

**SEHEMU YA PILI**
UCHAMBUZI WA KUJIKOSOA KAMA CHAMA …………………. 8-21

**SEHEMU YA TATU**
KUJENGA MSINGI WA UCHUMI WA KIJAMAA WA
TAIFA LINALOJITEGEMEA ……………………………………….. 22-40

**SEHEMU YA NNE**
CHAMA NA MAPINDUZI YETU ……………………………………. 41-59

# DIBAJI

Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama katika Mkutano wake uliofanyika mjini Dar es Salaam kuanzia tarehe 23 Novemba, 1981 hadi tarehe 7 Desemba, 1981 ilipitisha MWONGOZO WA CHAMA CHA MAPINDUZI wa 1981. Halmashauri Kuu ya Taifa ilifikia uamuzi huu baada ya kuzingatia na kuchambua hali halisi ilivyo hivi sasa nchini katika masuala ya siasa, uchumi na maendeleo ya jamii, na kuona kuwa kuna haja sasa ya kutoa msukumo mpya wa ujenzi wa Ujamaa, pamoja na utekelezaji sahihi wa maamuzi mengine mbalimbali yaliyokwisha kutolewa. Shabaha ya Mwongozo wa 1981 ni kufafanua kwa upana zaidi nadharia ya Chama juu ya masuala muhimu na ya msingi ya Siasa yetu katika fani mbalimbali, pamoja na kutoa maelekezo yaliyo wazi zaidi kuhusu mbinu sahihi za utekelezaji wa siasa hiyo.

Katika kipindi kilichofuatia kutangazwa kwa Azimio la Arusha, Chama kilitoa maandishi muhimu kadhaa yanayochambua na kufafanua fani mbalimbali za Siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea, pamoja na kuelekeza njia sahihi za utekelezaji wa siasa hiyo. MWONGOZO WA TANU wa mwaka 1971 ni miongoni mwa matamko hayo muhimu ya kipindi hicho. Mwongozo huo wa TANU unabaki na nafasi yake maalum katika historia ya mapambano ya Chama katika kusukuma mapinduzi ya Tanzania na Afrika kwa jumla katika kipindi hicho.

# SEHEMUYA KWANZA

## UTANGULIZI

1. Historia ya Watanzania kwa vile ni sehemu tu ya historia kubwa zaidi ya Waafrika kwa jumla lazima wakati wote ichambuliwe na kueleweka katika mazingira ya umoja wa Afrika na watu wake. Waafrika wamepitia vipindi na karne za fanaka na maendeleo ya jamii na pia vipindi na karne za misukosuko mikubwa na hata unyonge kitaifa.

2. Historia ya Waafrika ina mifano ya dola zilizofikia hatua kubwa ya maendeleo, ustaarabu na fanaka katika sehemu mbalimbali za bara hili na kwa nyakati mbalimbali. Maandishi, magofu, zana na mabaki ya vifaa vya aina mbalimbali vinavyogunduliwa sasa na wataalamu katika sehemu mbalimbali za Afrika vinathibitisha ustaarabu wa wakati huo katika fani za kilimo, ujenzi, vita, biashara na siasa.

3. Historia ya bara hili pia ina kumbukumbu za vipindi vya misukosuko ya kuingia kwa mataifa ya kigeni . Kuna kipindi Waasia walipoingia Afrika kwa madhumuni ya kujinufaisha na biashara walizoendesha humu Afrika. Mojawapo ya biashara haramu walizoanzisha ni biashara ya watumwa ambayo ilienea hata hapa Tanzania. Biashara ya Watumwa katika Afrika iliendeshwa pia na mataifa ya Ulaya. Inakisiwa kuwa Waafrika wapatao milioni mia moja walihusika na biashara hii ya utumwa. Kumbukumbu za kipindi hiki ambacho watu walisakwa, walikamatwa na kuuzwa bado zingali hai miongoni mwa Watanzania.

4. Kipindi kilichofuatia ni cha wakoloni wa mataifa ya Ulaya waliowanyang'anya Waafrika ardhi yao, kuigawa na halafu wakawatawala. Wakati huu Watanzania walitumikishwa na wakoloni. Mazao na matunda ya jasho lao yalichukuliwa kupelekwa nchi za wakoloni kujenga uchumi wao.

5. Watanzania, kama ilivyokuwa kwa Waafrika wengine kote barani Afrika, hawakukiri uvamizi, utumwa wala kutawaliwa bali walisimama imara kupambana na maadui kwa vita na mbinu nyingine.

6. Ni vigumu hapa kueleza kwa undani mifano yote ya mapambano ya Watanzania dhidi ya uvamizi wa kikoloni. Hata hivyo ni muhimu kutaja mifano michache ambayo ni vilelezo vya ushujaa, moyo wa uzalendo na jeuri ya kukataa kutawaliwa: vita vya Wasambaa chini ya Kimweri, vita vya Wahehe vikiongozwa na Mkwawa, vita vya Maji Maji vikiongozwa na Kinjeketile, Mputa na Kibasila. Wakati huo huo Waafrika wa Zanzibar walipambana kuupinga uvamizi uliofanywa na Waarabu ambao baadaye walishirikiana na ukoloni wa Waingereza. Watanzania wakati huo hawakufanikiwa kuwang'oa wakoloni.

7. Kushindwa kwa Waafrika katika mapambano hayo kunaelezeka. Kwanza ni kwa sababu Waafrika hawakuwa na umoja, walikuwa wamegawanyika katika makabila ambayo yaliishi kwa kutiliana mashaka, kushambuliana na kudharauliana. Wavamizi waliuelewa mfarakano huu na walitumia laghai za aina mbalimbali ili kuwagawa zaidi na kuwashinda mmoja mmoja. Pili zana za vita za Waafrika wakati huo zilikuwa hafifu ukilinganisha na silaha bora zaidi za wavamizi. Na Tatu ni kuwa sababu ya kwanza na ya pili zilifanya upeo wao wa kuandaa malengo na mbinu za vita uwe mfinyu sana na ambao ulitegemea zaidi ushupavu na ushujaa kuliko kuchambua uhusiano wa nguvu kati yao na adui na kutambua nguvu na udhaifu wao na nguvu na udhaifu wa adui ili kuvitumia vipengele hivyo kwa maslahi yao.

8. Miaka iliyofuatia Vita vya Maji Maji ilikuwa ya misukosuko na matatizo makubwa kwa wananchi. Pamoja na unyonge wa watu waliopoteza maelfu ya ndugu zao, miaka hiyo ilikuwa na janga la njaa na magonjwa ya kuambukiza, hasa ndui.

9. Wakati huo huo maelefu ya watu walilazimishwa kuutumikia ukoloni kwenye ujenzi wa Reli ya Kati na ya Tanga na kazi nyingine za harubu ambako walikumbana na ukatili wa Wajerumani usioelezeka. Katika Vita Vikuu Vya

Kwanza Vya Dunia wananchi walilazimishwa kushirikiana na wakoloni wa Kijerumani au wa Kiingereza kutetea ukoloni na kwa mara nyingine tena wengi walipoteza maisha yao katika vita visivyokuwa vyao.

10. Lakini, pamoja na haya vuguvugu la kisiasa liliongezeka. Haikupita miaka mingi baada ya Vita Vikuu vya Kwanza ishara za kwanza zilijitokeza Bara na Visiwani. Mwaka 1929 Waafrika walianzisha African Association kwa Bara ambayo mwaka 1948 ikajiita Tanganyika African Association na 1934 walianzisha African Association Visiwani, vyote vikiwa vyama vilivyojishughulisha na ustawi wa jamii pamoja na utetezi wa maslahi fulani fulani ya Waafrika.

11. Mwisho wa Vita Vikuu vya Pili ulifuatiwa na vuguvugu la mwamko wa kisiasa ulioongezeka kutokana na hali ya ukoloni nchini kuwakera na kuwabana mno wananchi pamoja na vuguvugu la askari waliorudi toka mpakani.

12. Wakati huo huo, kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi bandarini na Serikalini na siasa ya ubaguzi wa rangi na ya mishahara iliyoendeshwa na watawala wa Kiingereza kuliwatia wafanyakazi dukuduku la kutaka kuungana na kupigania haki zao. Mgomo mkubwa wa kwanza wa makuli wa Dar es Salaam na pia Zanzibar uliowatikisa wakoloni ulitokea kunako mwaka 1948. Hali ilikuwa inajiandaa kwa uwezekano wa kuanzishwa vyama halisi vya kisiasa nchini.

## A. KUZALIWA KWA TANU NA ASP

13. Historia ya sasa ya mapambano ya ukombozi katika Tanzania ni historia ya vyama vya kisiasa vya TANU na ASP. Tanganyika African Association na African Association na Shirazi Association kwa Zanzibar vilianzisha vuguvugu la siasa na kuandaa mazingira ya kuviwezesha vyama kamili vya kisiasa kujitokeza. Vuguvugu la vyama vya wafanyakazi nalo liliongezea joto la kisiasa nchini. Wakati huo huo nchi nyingine kama Ghana ya Kwame Nkrumah na Kenya ya Jomo Kenyatta, zilikwisha anza kuunda vyama vya kuongoza mapambano ya uhuru, na vuguvugu lake liliongezea mwamko wa uhuru wa Watanzania.

14. Hivyo, TANU (7.7.54) na ASP (5.2.57) viliundwa na kujipa majukumu ya mashujaa wa Maji Maji na wengineo walioshindwa huko nyuma na kujibunia malengo, mbinu na zana mpya kwa madhumuni yale yale ya kuung'oa ukoloni wa Kiingereza nchini Tanzania Bara na usultani na uwakala wa Kiingereza Visiwani Zanzibar. Mapambano yalikuwa makali na magumu Tanzania Bara na Visiwani.

15. TANU, chini ya uongozi wa Mwalimu Julius K. Nyerere, ilifaulu kuwaunganisha Watanganyika kwa jumla katika hali ngumu ya ukabila, hila, vitisho na mbinu za Serikali ya Kiingereza. TANU iliyafikisha mapambano ya uhuru hadi kwenye uwanja wa kimataifa na Umoja wa Mataifa ambako hila za ukoloni wa Kiingereza zilifichuliwa na kushindwa. Vyama kadhaa vilivyozushwa ili kuwagawa Waafrika na kuchelewesha uhuru vyote vilishindwa. Uingereza ilibidi ikiri nguvu na sauti ya TANU na tarehe 9 Desemba, 1969 Tanganyika ilijinyakulia uhuru wake, miaka saba tu baada ya kuundwa kwa Chama hicho.

16. Afro-Shirazi Party, chini ya uongozi wa Sheikh Abeid Aman Karume, kilikua mwaka hadi mwaka na kuvishinda vyama vingine vyote vya upinzani. Lakini dola ya Sultani kwa kushirikiana na ukoloni wa Uingereza walikinyang'anya Chama cha Afro-Shirazi ushindi wake wa halali katika Uchaguzi Mkuu mara nne mfululizo. Ndipo tarehe 12.1.1964 Chama Cha Afro-Shirazi kikafanya mapinduzi halali ya silaha yaliyoitokomeza Serikali haramu ya Sultani mwezi mmoja baada ya Sultani na vibaraka wake wa Nationalist Party kukabidhiwa uhuru wa bandia na Waingereza.

17. Vyama vya TANU na ASP vilijenga historia ya kushirikiana na kuunga na mkono tangu kuundwa kwao. Kwa hiyo, mara baada ya mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya TANU iliyatambua mapinduzi hayo na kuyaunga mkono kwa vitendo. Miezi mitatu baada ya mapinduzi ya Zanzibar ushirikiano na udugu wa jadi wa wananchi wa Zanzibar uliimarishwa kwa kitendo cha kimapinduzi cha kuunganisha nchi mbili hizi katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao sasa unaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## B. MAPAMBANO YA KULINDA UHURU NA KUJENGA JAMII MPYA

18. Serikali ya Mapinduzi ya ASP haikuchelewa kuchukua hatua za kuimarisha ushindi iliyoupata dhidi ya usultani. Hatua muhimu katika fani za siasa, uchumi na ustawi wa jamii zilichukuliwa kama msingi wa kwanza katika kazi ngumu ya kuijenga jamii mpya ya haki na usawa. Ardhi ilitaifishwa na hodhi kubwa za makabaila wa kiarabu waligawiwa umma wa wananchi wasiokuwa na ardhi. Wakati huo huo mabenki na biashara ya nje zilitaifishwa na vyombo vya umma kuundwa.

19. Serikali ya TANU haikuchelewa kuchukua hatua za dhati za kujiimarisha ili kuikabili kazi kubwa ya kulinda uhuru na kuanza ujenzi wa uchumi na wa jamii mpya inayojitawala katika hali ya matazamio makubwa ya wananchi kwamba uhuru utawaletea mabadiliko ya haraka katika hali ya maisha yao. Miaka mitano ya kwanza iliyofuatia uhuru ilikuwa kipindi kigumu kwa TANU na Serikali yake changa. TANU yenyewe ilibidi iondokane na hali ya kuwa Chama cha kupigania uhuru na kuwa Chama cha kulinda uhuru na kujenga Taifa linalojitawala. Wakati huo huo Chama kiliwajibika kuiongoza Serikali na wananchi kwa jumla katika jitihada ya kutafuta falsafa ya jamii itakayolingana na matazamio ya wananchi na inayoweza kuwaletea maendeleo halisi nchini.

20. Ilidhihirika katika miaka hiyo ya mwanzo ya uhuru wa Tanganyika kuwa mgongano ulianza kujengeka kati ya matazamio ya wananchi jumla kwamba uhuru ungaliwaletea mabadiliko katika hali ya maisha yao na kwa haraka, na uwezo mdogo wa Serikali wa kukidhi haja za wananchi kulingana na matazamio yao. Mabadiliko makubwa ya mapato na hali ya maisha yaliyoonekana kwa wachache, viongozi na maafisa wa madaraka yaliyokuwa yanashikwa na wakoloni zamani, pamoja na vitendo vya baadhi ya viongozi na maafisa hawa vya kuanza kutumia nafasi zao kujitajirisha, viliimarisha mgongano huo. Tafsiri ya hali hii ilijitokeza wazi wakati umma ulianza kuwaita wale walioonekana wanafaidika kwa vyeo vya uhuru "Naizesheni" wakati wananchi waliobaki kuitwa Baba kabwela".

21. Pamoja na misuguano hii ya kijamii, uongozi wa Chama ulianza kuwa na wasi wasi na maendeleo ya kiuchumi yaliyopatikana tangu uhuru. Maongozi ya uchumi wakati huo yalikuwa kwamba msingi wa maendeleo ya nchi ni rasilimali toka ng'ambo. Ilianza kudhihirika kuwa utekelezaji wa msimamo huo kiuchumi haukuwa na matokeo yaliyotarajiwa.

22. Katika hali hiyo ambapo Chama kilianza kuona kuwa Serikali yake inashindwa kutosheleza matazamio ya wananchi kwa jumla na badala yake kukabiliwa na ongezeko la misuguano ya kijamii mijini na vijijini, na ambapo kilianza kuingiwa na mashaka na kutoridhika na matokeo ya utekelezaji wa mipango ya uchimi wa taifa uliotegemea rasilimali toka ng'ambo kuwa ndiyo msingi wa maendeleo, Chama kiliwajibika kujiuliza maswali juu ya usahihi wa siasa ambayo kimeifuata na kuitekeleza tangu nchi ijipatie uhuru. Siasa ya uchumi ya kipindi hiki ilikuwa na sura mbili: kujenga nchi kwa msingi wa ubebari na kwa kutegemea rasilimali toka ng'ambo. Funzo tulilopata kama Chama ni kuwa siasa hiyo ya uchumi ilikuwa imeshidwa kwa maana mbili: Kwanza ni kuwa badala ya kusaidia kuimarisha umoja wa Taifa ulioanza kujengwa wakati wa kupigania uhuru ilizalisha migongano ya kijamii na kuanza kukifarakanisha Chama na umma. Pili, Siasa hiyo ya uchumi wa kibepari unaotegemea rasilimali toka ng'ambo kama msingi wa maendeleo hayo pia ilishindwa maana utekelezaji wake hakuleta vuguvugu la maendeleo ya kiuchumi yaliyotegemewa na wala hakukuwa na mtiririko wa rasilimali za kutosha toka ng'ambo kuingia nchini.

## C: AZIMIO LA ARUSHA

23. Tangu nyakati za kupigania uhuru Chama kiliweza wakati wote kuelewa na kutambua mwenendo wa hali ya mapambano nchini na duniani kwa jumla na kuchukua hatua sahihi kwa wakati unaofaa ili kuimarisha na kuendeleza mapambano ya wananchi. Kuna maamuzi kadhaa katika historia ya Chama chetu, ambayo ni pamoja na uamuzi wa kuunganisha nchi za Tanganyika na Zanzibar yanayoonyesha kinaganaga uwezo huo wa Chama kukua na nyakati.

24. Kielelezo kimoja kikubwa cha uwezo wa Chama kukua na nyakati na kuelewa mahitaji halisi ya maendeleo ya mapinduzi ya umma ni Azimio la Arusha juu ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Kwa uamuzi huo, msingi mipya na ya kimapinduzi ya kulijenga na kulilinda Taifa iliwekwa hadharani. Kutaifishwa kwa mabenki, biashara ya nje na mashamba makubwa ya mabepari, kuundwa kwa mashirika ya umma na kuanzishwa kwa viwanda vya umma ni baadhi tu ya mambo yaliyodhihirisha nia ya Chama ya kuunda mfumo mpya wa uchumi utakaofanana na jamii ya kijamii inayodhamiriwa kujengwa.

25. Hatua za kujenga ujamaa zilizochukuliwa hadi sasa zimejenga msingi unaotia moyo na ni mafanikio ya kujivunia. Njia muhimu za uchumi kama benki, viwanda, biashara ya nje na ya ndani. Mashamba makubwa reli na posta zinamilikiwa na umma, tofauti ya mishahra kati ya iliyokuwa chini kabisa na iliyokuwa juu kabisa Serikali wakati wa kupata uhuru ilikuwa ya uwiano wa 1:7. Pamoja na hali ya uchumi wetu kitaifa kuwa ya matatizo, tumefaulu kutoa elimu bure toka msingi hadi Chuo Kikuu na elimu kwa watoto wote wa kiwango cha msingi; wakati huo huo tunatoa matibabu bure toka vijijini hadi mijini; wananchi wana nafasi ya kushiriki katika mambo yanayowahusu, wafanyakazi wana mabaraza yao, wakulima vijijini wana Serikali zao zinazoendesha shughuli zao wakati mpango wa demokrasia ya Chama kimoja unawapa nafasi wananchi kuchagua wabunge wao. Yote haya na mengine ni vielelezo vya mafanikio ya Siasa ya Ujamaa. Aidha, uwezo tuliouonyesha kwa kukabiliana na shida kubwa ya njaa mwaka 1974/75 bila Watanzania kupoteza maisha yao na pia ushindi wetu dhidi ya majeshi ya uvamizi ya Iddi Amin ambao umepatikana kutokana na mshikamano sahihi wa Chama, Serikali, wananchi na wapiganaji, yote haya ni mafanikio ya ujamaa.

26. Tungeweza kuendelea kukariri mafanikio yaliyopatikana nchini kutokana na utekelezaji wa siasa ya Chama ya Ujamaa na Kujitegemea. Lakini jambo la kuzingatia ni kuwa hatua tulizozichukua katika kutekeleza Siasa ya ujamaa na Kujitegea ni za awali tu na kwamba kubwa zaidi tulilofanikiwa ni kujichorea barabara tunayodhamiria kufuata katika kulijenga Taifa letu la watu sawa na huru ambalo lengo lake ni maendeleo kwa wote.

# SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA KUJIKOSOA KAMA CHAMA:

### (1) Upungufu katika kusimamia uchumi

27. Halmashari Kuu ya Chama ya Taifa katika kikao chake cha tarehe 15 hadi 17 Mei, 1981 ilizingatia hali ya uchumi na jamii inayolikabili Taifa na kufanya uchambuzi ili kubainisha kiini cha matatizo haya. Uchambuzi uliofanywa ulidhihirisha mambo makubwa matatu. Kwanza, ni kwamba matatizo ya kiuchumi yanayoikabili nchi yetu si ya kipekee kwa Tanzania kwa Tanzania bali ni matatizo yaliyozikumba nchi zilizoendelea, zilizoamua kujenga ujamaa na zile zilizoamuma kujenga ubebari.

28. Jambo la pili lililodhihirika ni kuwa baadhi ya sababu za matatizo yetu ya kiuchumi ziko nje ya uwezo wetu. Mfumo wa biashara ya kimataifa ulivyo unazikandamiza na kuzinyonya nchi changa kama Tanzania. Kwa mujibu wa mfumo huu wa biashara ya kimataifa nchi za viwanda zinajipangia bei za bidhaa za viwanda vyao na kutuuzia sisi na wakati huo huo nchi hizo hupanga wao bei za mazao ya kilimo tunayozalisha sisi na kuwauzia. Vile vile Tanzania haina kauli na bei za mafuta tunayoyaagiza toka ng'ambo.

29. Sasa, bei za mafuta na bei za bidhaa za viwanda vya nchi zilizoendelea zimepanda sana katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Tanzania sasa inawajibika kutumia asilimia sitini ya mapato yake yote ya fedha za kigeni kununulia mafuta ambapo mwaka 1972 ilitumia asilimia kumi ya fedha za kigeni kununua kiasi hicho hicho cha mafuta. Wakati huo huo, kwa kutumia mbinu za kupandisha bei za bidhaa zao za viwanda na kushusha bei za mazao ya nchi changa, nchi zilizoendelea zimefaulu kuupunguza kabisa uwezo wetu wa kununua bidhaa za viwanda vyao zinazohitajika sana na nchi changa. Kwa

mfano, miaka kumi iliyopita Tanzania iliweza kununua trecta moja toka ng'ambo kwa hamani ya tani tano za chai iliyouzwa ng'ambo. Leo Tanzania inahitaji tani kumi na saba za chai ili kununua trecta la aina ile ile. Hali hii lazima iwe na matokeo mabaya kwa uchumi wa Taifa letu.

30. Nchi yetu pia imepatwa na matatizo ya ndani ambayo pia tusingekuwa na uwezo wa kuyazuia na yotete yameathiri hali yetu ya uchumi. Matatizo hayo ni pamoja na vita vya kujihami tulivyolazimika kupigana dhidi ya majenshi ya uvamizi wa Iddi Amin, mafuriko makubwa ya 1978/79 na hali ya ukame katika baadhi ya mikoa.

31. Jambo la tatu lililodhihirika vile vile ni kwamba sisi wenyewe kama taifa hatukutumia kwa kiasi cha kutosha nguvu za Chama, Serikali na za wananchi katika kutatua matatizo ya uchumi ambayo ufumbuzi wake tuna uwezo nao.

32. Jambo la kwanza linahusu kilimo kwa jumla. Pamoja na kuwa bei za mazao yetu tuyauzayo ng'ambo imekuwa ikishuka, mapato ya fedhs za kigeni kwa Taifa kutokana na mazao yanategemea pia kiasi taifa linachozalisha na kuuza. Taifa linalozalishakidogo litauza kidogo na kupata fedha chache za kigeni. Likizalisha mazao kwa wingi na kuuza litapata fedha za kigeni zaidi. Lakini, utoaji wa karibu mazao yetu yote ya biashara umepungua ukilinganisha na miaka ya nyuma. Ni dhahiri kuwa hata kama tumekuwa na matatizo ya mafuriko na ya ukame hapa na pale, hushindwa kwwetu kuongeza utoaji wa mazao ya biashara na chakula kunatokana pia na kushindwa kwetu kuwaongoza wananchi kwa maandalizi thabiti, mipango na msukumo katika kilimo.

33. Pili kuna suala la utengenezaji mali wa kijamaa. Laiti kama Chama kingeongoza, kusimamia, kuhimiza na kusaidia utekelezaji wa Ujamaa Vijijini vizuri tangu Azimio la arusha hadi sasa, tungeweza kuwa na sekta kubwa ya ujamaa katika kilimo vijijini ambavyo ingetuwezesha kutoa ziada ya mazao ya chakula na biashara kuliko ilivyo sasa. Kama wastani wa ekari za ujamaa wa kila kijiji nchini ungekuwa angalau ekari mia kwa kila kijiji wakati huu basi sekta ya ujamaa

vijijini kaktika kilimo ingekuwa na ekari zipatazo laki sita. Ekari laki sita za ujamaa zingeweza kuongeza ziada ya mazao yanayotolewa na Taifa kwa kiasi kikubwa.

34. Na tatu ni kuwa jitihada zetu za kuunda na kupanua sekta ya umma haikuambatana na jitihada ya kutosha ya kuaelimisha, kuwaandaa na kuwajenga wafanyakazi na viongozi wa kazi katika misingi ya kufanya kazi kwa nidhamu na ari, misingi ya uzalendo na ya uaminifu kwa umma. Hali hii imeathiri utengnezaji mali na utoaji huduma wa sekta hii. Viwanda vingi nchini havitoi mali kwa kadri ya uwezo vilio nao na pia mali nyingi ya umma hupotea kutokana na vitendo vya wizi, uzembe na ubadhirifu. Upungufu wetu katika kujenga maadili ya kijamaa. Miongoni mwa wafanyakazi na wakuu wa kazi ni moja ya sababu zilizofanya viwanda na mashirika yaliyo mengi nchini yasitoe mchango wa kutosha katika kuujenga uchumi wa taifa.

35. Lakini maadui wa ujamaa wa nje na wa ndani wanaeneza kuwa matatizo yetu yanatokana na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Maadui hawa wa ujamaa wanajua kuwa wayasemayo si kweli, lakini kwao wao kukashifu ujamaa ni sehemu muhimu ya mbinu zao za vita vya ghiliba dhini ya Ujamaa. Kwani ukweli unaojitokeza wazi wazi ni kuwa baadhi ya matatizo yetu ya uchumi yanatokana na kutotekeleza kwa dhati Siasa ya ujamaa na Kujitegemea vijijini na katika sekta ya umma tuliyoianzisha. Zaidi ya hivyo, wakati mwingine katika miaka kumi na mnne tangu Azimio la arusha, Chama, Serikali na vyombo vyake vimetumika kukuza sekta ya kibepari nchini katika viwanda, biashara, usafirishaji, ujenzi na kadhalika na ubepari huo uliopanuka katika kipindi hiki umeimarisha vitendo vya kuivuruga na kuidhoofisha sekta yetu ya Umma.

36. Aidha, kuna matatizo ya kijamii kama vile kuongezeka kwa rushwa, hujuma za kiuchumi, wizi, ujambazi na uharibifu w mali ya umma, mambo ambayo yanatupunguzia nguvu zetu za kiuchumi na kudhoofisha dhamira ya umma ya kujenga ujamaa. Haya yote yamo katika uwezo wa Chama, Serikali na wananchi kuyapiga vita na kuyashinda.

37. Hivyo, katika kufanya uchambuzi wa kujikosoa, Halmashauri Kuu ya Chama ya taifa ya Mei, 1981 ilikiri kuwa pamoja na kwamba Chama chetu, tangu TANU na ASP hadi sasa Chama Cha Mapinduzi kimepata mafanikio na ushindi wa kihistoria katika nyanja mbalimbali za mapambano, ni muhimu kukubali pia kwamba kimeonyesha upungufu usiokatalika, kama chombo kikuu cha uongozi wa Taifa na hasa chombo cha uongozi wa harakati za kujenga ujamaa na Kujitegemea nchini. Kukiri upungufu huu si kitendo cha kujidhoofisha bali ni kitendo cha kujiamini na kujiimarisha.

### (1) Wana CCM ndiyo askari wa mstari wa mbele wa mapambano ya kujenga Ujamaa.

38. Uchambuzi wa kujikosoa umedhihirisha kuwa kwa miaka mingi Chama hakikuthamini ipasavyo uanachama na kuitambua nafasi ya wanachama katika harakati za ujenzi wa ujamaa na wa Taifa kwa jumla. Chama cha kimaa kama CCM ni chombo cha kuongoza mapambano ya ujamaa nchini. Ni kweli kuwa ujamaa kimsingi ni siasa ya Wakulima na Wafanyakazi na kwamba utajengwa na wafanyakazi katika umoja wao wa kitabaka. Lakini ni kweli pia kwamba bila ya wapiganaji ujamaa wa mstari wa mbele, bila kikosi cha askari wa mstari wa mbele kujenga ujamaa haliwezi kufikiwa. Kikosi hicho cha wapiganiaji ujamaa wa mstari wa mbele ni wanachama wa Chama Cha Mapinduzi.

39. Vyama vyetu asilia, ASP na TANU, vilifaulu kuwawezesha wanachama wake kuwa kikosi thabiti cha mstari wa mbele cha kupigania uhuru. Wanachama hao kwa jumla walijitolea mhanga kwa ajili ya mapambano ya uhuru wa nchi yao, mapambano yao waliyaweka kabla ya maslahi yao binafsi na mengine yoyote. Tutakuwa tunajidanganya tukisema kuwa anachama wote wa Chama cha Mapinduzi na pia wanachama wote wa TANU na ASP katika miaka kadhaa kabla ya kuundwa kwa CCM, walikuwa kikosi kinachotimiza sifa hizo kwa upande wa lengo la kujengauJAMAA. Mapambano ya uhuru yalikuwa ya wenyewe, wanaTANU na wanaASP wa enzi hizo, na kuwa wananchi waliobaki walielimishwa, walihamasishwa na walishirikishwa katika mapambano ambayo

chimbuko la vuguvugu lake lilikuwa msimamo na vitendo vya wanachama. Katika maana hiyo, mapambano ya kujenga Ujamaa Tanzania lazima yawe na wenyewe.

40. Hali hii haikuzuka siku moja bali ni matokeo ya msimao na vitendo vya miaka mingi. Ilianza tangu baada ya uhuru, wakati viongozi wa ngazi ya taifa, Mkoa na Wilaya hawakuipa uzito kwa vitendo nafasi ya mwanachama katika mapambano yetu. Karibu viongozi wote tulishughulika na mikutano ya hadhara, mikutano ya wananchi kwa jumla bil aya kujali kukutana na wanachama. Viongozi wengine wa Chama tulilemazwa na umangi meza na wengine hata kufikiri wangeimarisha utekelezaji wa shughuli za Chama kwa njia ya vyombo vya habari tu. Ingewezekana kwa viongozi kuhakikisha kuwa kila baada ya mikutano ya hadhara ya wananchi wote, ambayo pia ina umuhimu wake, wanakutana na wanachama wenzi wao ili kuulizia juu ya hali ya Chama mahali hapo na pia kuonyesha kuwa uanachama ulikuwa namaana na uzito maalum ambao viongozi wanautambua. Lakini hatukufanya hivyo na matokeo yake ni kwamba fikra zilijengeka kuwa uananchi ulikuwa unatoshs kabisa.

41. Jwa wanachama walio wengi wa CCM kutokuwa kikosi cha mstari wa mbele cha kupigania ujamaa na kutojiona kuwa ndiyo wenye mapambano ya kujenga ujamaa kumetokana pia na ukweli kuwa Chama hakitakuwa na mpango wa kuwajenga na kuwaandaa wanachama kwa madhumuni hayo. Mwamko wa kitaifa na wa kizalendo ulikuwa rahisi kumpata Mwafrika wa Tanzania wakati wa ukoloni maana adui, ambaye ni mtawala wa kigeni, alikuwa anaonekana waiz wazi na hivyo suala la fedheha ya kutawaliwa ililkuwa rahisi kulieleza na rahisi pia kueleweka na kumkera mtu. Uadui wa mfumo wa kibepari ni mgumu zaidi kuuelezea mpaka ueleweke na kumtia mtu mori ya kuuchukia na kuukataa. Ubepari au unyonyaji si suala la rangi ya mtu na hivi sasa baadhi ya wanyongyaji nchini ni Waafrika wenzetu. Kwa hiyo, wanachama wa Chama cha kujenga ujamaa wanahitaji zaidi maandalizi ili waelewe uzito w mapambano na kupata mbinu za kuongoza mapambano ya umma kwa vitendo. Viongozi wanahitaji maandalizi ya hali ya juu zaidi.

42. Hali hii ambapo wanachama na vionozi kwa jumla waliachiwa wajitetee wenyewe (na wengine wametimiza wajibu wao kwa sifa) iliimarisha hali iliyozungumziwa hapo awali kwamba uanachama na uananchi ulikuwa sawa tu na hivyo suala la nani amwongoze nani lilijitokeza maana kama kuongoza ni kuonyesha njia basi haikuweza kuwa dhahiri wote kuhusu nani aijuaye njia, ni mwanachama wa CCM au mwananchi kwa ujumla, ni viongozi wa CCM au wanachama.

43. Vyo vya chama ambavyo ndivyo ingebidi viwe mahala pa kuandaa wanachama hasa viongozi wa Chama vimeendelea kuwa vyuo vya Elimu ya Siasa kwa jumla. Ni kweli kuwa Chama chochote cha kijamaa halisi lazima kiwe na mipango thabiti ya kutoa elimu ya siasa ili kuwahamasisha wananchi kwa jumla na hasa makundi ya taasisi mbalimbali kama vyuo, shule, majeshi, vijana, wafanyakazi, wakuu wa kazi na kadhalika. Lengo la elimu ya siasa kwa taasisi hizi ni kuuinua mwamko wao wa siasa na kuwapa wahusika mwelekeo wa kisiasa kwa kulingana na shughuli zao katika nchi. Lakini wanachama wanahitaji mafunzo ya siasa ya Chama ili kuongeza upeo wao wa kuielewa siasa ya ujamaa, mafunzo ya mbinu za kushiriki na kuongoza umma mahali walipo katika harakati za kujenga ujamaa na mafunzo ya kuwapa uwezo wa kueneza na kutetea siasa ya Chama. Mafunzo haya hutolewa na vyuo vya Chama utaratibu na malengo yaliyo wazi.

### (3) **Umuhimu wa nadharia sahihi ya Ujama**

44. Pamoja na upungufu wetu kama Chama kuhusu nafasi ya uanachama na wanachama katika mapambano yetu ya kujenga ujamaa kuna suala linalohusu umuhimu wa nadharia sahihi ya Chama. Chama ni muungano wa watu wanaokubaliana juu ya lengo katika jamii na namna ya kulifikia. Kinachowaunganisha ni fikra zao, itikadi yao, inayohusu jinsi gani shughuli za jamii nchini ziendeshwe na kwa maslahi ya nani. Ni muhimu kusisitiza kuwa kinachowaunganisha wanachama ni itikadi, fikra na falsafa yao ya siasa.

45. Lakini masuala ya falsafa, itikadi na fikra ni masuala ya nadhari. Hivyo suala la nadharia ya Chama ni suala la msingi kabisa kwa uhai wa Chama, kwa

maendeleo ya mapambano ya Chama, kwa malengo na mbinu za mapambano hayo na kwa umoja, nguvu na usahihi wa vitendo vya Chama na vya wanachama.

46. Chama chetu ni miongoni mwa vyama vichache katika Afrika ambavyo vimefaulu kubuni nadharia ya ujamaa iliyo sahihi, wazi na ya kiwango cha juu. Nadharia hiyo ya Chama inajidhihirisha yenyewe katika Katiba, Azimio la Arusha, Mwongozo na maandishi mengine muhimu ya Chama. Nadharia hii ya siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea imetujengea msingi wa uelewano, umoja na ushirikiano wa aina mpya katika ujenzi wa taifa na kutufanya tueleweke na wengi kimataifa, jambo ambalo limetupa sifa na heshima duniani kote.

47. Tumetamka hapo awali katika kujikosoa kuwa siku za nyumba tumeonyesha upungufu kwa kutokuwa na mipango thabiti ya kuwaandaa wanachaa na hasa viongozi. Upungufu huu umekuwa na matokeo kwa upande wa nadharia. Pamoja na nadharia fasaha iliyomo katika maandishi maku ya Chama, pamoja na jitihada na uwezo wa Mwenyekiti wa Chama Mwalimu J.K Nyerere, wa kufafanua na kuendeleza nadhari ya Chama, viongozi wengi tumetosheka na kiwango kisichoridhisha cha nadharia. Wengine tumediriki hata kuipiga vita nadharia na kupuuza umuhimu wa kujifunza siasa na nadharia ya Chama, kuinua uwezo wetu wa uchambuzi wa masuala mbalimbali ili kuweza kutetea na kueneza siasa ya Chama kwa hoja, uchambuzi na ufafahuzi ulio wazi na sahihi.

48. Ni muhimu kusisitiza kuwa pamoja na maandishi ya Chama yaliyo sahihi na ya kimapinduzi, pamoja na upeo na uwezo mkubwa alionao Mwenyekiti, mwalimu J.K. Nyerere, wa kutafakari na kuchambua masuala mbalimbali kwa kina na ufasaha au wa kiongozi mwingine yeyote, lakini kwa kuwa Chama ni wanachama na viongozi wote kwa pamoja katika mshikamano wao wa nadharia na vitendo, basi ni hatari kwa maendeleo ya Chama na ya siasa yake ya ujamaa kuiachia hali ambapo kiwango cha kuielewa nadharia ya Chama kinahitilafiana mno kati ya wana CCM na hata kati ya viongozi wa ngazi moja ya uongozi.

49. Chama chetu kinaongoza mapambano ya Watanzania katika mazingira ya Watanzania katika mazingira ya kimataifa yaliyo magumu na yenye sura nyingi katika siasa, uchumi na jamii. Kuweza kuliongoza Taifa katika mazingira haya magumu, Chama kinahitaji kuwa na uwezo wa juu wa kuyaelewa mazingira hayo ambayo hayawezi kueleweka bila ya uchambuzi wa kina na nyenzo za kufanyia uchambuzi huo. Uchambuzi huu lazima ukiwezesha Chama kufichua mvutano wa maslahi uliopo baina ya mataifa kufichua uhusiano halisi wa nguvu kati ya ubeberu na ubepari wa dunia kwa upande mmoja na nguvu za ujamaa kwa vuguvugu la ukombozi wa taifa kwa upande mwingine, na kufichua uhusiano halisi uliopo kati ya mataifa ya viwanda na mataifa yasiyo ya viwanda. Uchambuzi wa aina hiyo ndio utakaokiwezesha Chama kuliongoza Taifa kwa usalama kimataifa na kwa maslahi yetu.

50. Akati huo huo hali ya ndani ya Tanzania imebadilika sana. Uchumi wa taifa, huduma na jamii yenyewe yote imekuwa na kupanuk. Kuielewa vema jamii ya Tanzania ya leo kunataka uchambuzi wa hali ya juu pia. Uchambuzi huu ukiwezeshe Chama kuielewa migongano ya maslahi ya tabaka ambayo imejitokeza nchini. Migongano hii ina mizizi yake katika mgongano wa msingi kati ya ujamaa na ubepari, kati ya maslahi ya wakulima na wafanyakazi kwa upande mmoja, na ya ubinafsi ubwanyenye na ubepari ambao umekuwa ukijengeka tangu Azimio la Arusha kwa upande mwingine. Kwa hiyo, ili Chama kiweze kuendelea kuongoza mapambano ya kujenga ujamaa ni muhimu kuwa na uwezo wa kufanya uchambuzi sahihi wa hali ya jami yetu.

51. Jambo linalosisitizwa hapa ni kuwa kwa Chama Cha mapinduzi kuongoza ipasavyo siasa ya ndani na ya nje ya nchi yetu ni muhimu kwa viongozi wa ngazi zote na pia wanachama kuwa na uwezo wa hali inayoridhisha ya nadharia kama silaha katika kutekeleza jukumu hilo. Hivyo, ni jambo la umuhimu wa kwanza kwa viongozi na wanachama kujiendeleza katika nadharia ya siasa ya Chama. Kwa kiongozi au mwanachama wa CCM kupuuza, kudharau au kukataa kujiendeleza katika nadharia kwa visingizio vyovyote ni msimamo wa uhasama dhidi ya maendeleo ya Chama.

52. Ujenzi wa ujamaa si lelemama bali ni mapambano, mapambano ya kudumu dhidi ya ubepari na unyonyaji, dhidi ya wapinga maendeleo na wababaishaji wa kisiasa, dhidi ya wahujumu uchumi, majambazi, wezi, wazururaji na wazembe. Msimamo sahihi wa mapambano unaotokana na nadharia sahihi ya ujamaa ungelituepusha na maamuzi na vitendo ambavyo vimerahisisha kuoteshwa kwa mizizi ya ubepari, kinyume cha msimao wa mapambano dhidi ya ubepari. Leo ubepari, una vishawishi vingi zaidi nchini kuliko ulivyokuwa kabla ya Azimio la Arusha kwa sababu pamoja na kwamba sasa tuna sekta kubwa ya umma lakini kutokana na udhaifu wa kutopambana nao, ubepari umefaulu kujipanua na kujipenyeza hata ndai ya sekta yenyewe ya Umma. Na ndiyo maana ubepari sasa unathubutu kujitokeza hadharani kuukashifu ujamaa, kubabaisha baadhi ya viongozi na kututaka tubadilishe siasa yetu.

53. Upungufu wa nadharia ya ujamaa unaweza kuathiri maslahi ya Chama kwa namna nyingine. Chama cha kijamaa kama CCM ni chombo cha uongozi, si chombo cha amri na utawala wa mabavu. Kinaongoza kwa kuelimisha, Kuelewesha, kushauri, kushawishi, kushirikisha na kuelekeza na nguvu yake kubwa inatokana na kukubalika kwake na umma, mshikamano wa wanachama wake na fikra sahihi za siasa yake inayolingana na maslahi ya Umma, mshikamano wa wanchama wake na fikra sahihi za siasa yake inayolingana na maslahi ya Umma. Ili kutimiza jukumu lake la uongozi kinahitaji nguvu ya hoja siyo hoja ya nguvu. Hivyo, kiwango cha juu cha nadharia kinahitajika kwa viongozi wa ngazi zote na hata wanachama ili kuwaelimisha na kuwashawishi wasio wanachama, kuitetea siasa dhidi ya hujuma za maadui, kufafanua masuala mbalimbali na kujibu hoja za wanachama au wananchi kwa jumla. Kufanya ufafanuzi usioridhisha, kujibu hoja halali kwa juu juu au kuwaita waulizao maswali wapinzania wa Chama kama ifanyikavyo wakati mwingine khakujengi bali hudhoofisha Chama.

54. Katika kufnya uchambuzi wa kujikosoa katika Chama ni muhimu kuzingatia suala la uhusiano uliopo , mshikamano uliopo, kati ya nadharia na vitendo. Nadharia ina kazi ya kuangaza na kuongoza vitendo. Lakini kwa kuwa lengo la ujamaa I kuibadili dunia, kujenga misingi mipya ya uchumi, kuleta mfumo mpya wa jamii basi vitendo vya kijamaa ndicho kipimo cha ujamaa kwa Chama na ujamaa kwa Wanachama.

55. Suala hili la mshikamano wa nadharia na vitendo, la kutenda mapinduzi, linatusaidia kuelewa kwa undani mwenendo wa ujenzi wa ujamaa kama linavyohusu uamuzi wa kutaifisha na kazi ya kukibadili kilichotaifishwa kiwe chombo cha ujamaa. Kazi ya kuunda vyombo vya umma kama mabenki, viwanda, mashirika ya biashara, mashamba ya Taifa ni kazi nyingine muhimu ya kimajaa ni kuhakikisha kuwa ujamaa unajengwa ndani ya vyombo vya umma na hii imerahisisha fikra na tamaa za kibepari kuzagaa katika vyombo hivi na mwisho na kutekwa nyara ili vihudumie ubepari na ubinafsi.

56. Upungufu wa kuuelewa vilivyo uhusiano wa nadharia na vitendo katika harakati za ujamaa unaweza kusababisha pia msimamo usio sahihi wa kutenganisha jukumu la uongozi na utendaji au kazi. Uongozi si kazi ingawa zipo kazi za uongozi. Hivyo, wajumbe wa vikao vya Chama ni lazima wawe au na kazi zao za kawaida kama za ajira au kilimo ama wawe na kazi za uongozi katika Chama, Serikali aun Mashirika ya Umma. Vinginevyo kutakuwa na watu katika Chama ambao si wakulima wala si wafanyakazi na huu ndio mwanzo wa kujenga kundi la wababaishaji wa kisiasa, jambo ambalo ni hatari sana kwa harakati za ujamaa. Taifa ya kutenganisha uongozi na utendaji imeathiri maendeleo ya Chama kwa msukumo , usimamizi na utekelezaji maana kati ya uamuzi na utendaji kumekuwa hakuna kiungo.

57. Tatizo hili la kutenganisha uongozi na utendaji linaweza pia kukizorotesha Chama kwa kukifanya kisahau kuwa chenyewe vile vile ni mtendaji na kwamba kitapinmwa kwa vitendo vyake kama Chama. Katika maana hiyo Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi ipimwe na vikao vya juu kwa utekelezaji wake wa Siasa ya

Chama; kama wanachama wake wako mstari wa mbele kwa ujmaa, kama wanashiriki katika shughuli za kujitolea, kama wanashiriki katika shughuli za kujitolea, kama ni wafanyakazi hodari, kama kijiji chao kina maendeleo ya kijamaa na kadhalika. Vivyo hivyo kwa kamati ya utendaji ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Kwa hiyo, pamoja na kushughulikia uongozi wa serikali, Jumuiya na vyombo vingine, Chama kina kazi ya kujijenga chenyewe ili kujipa uwezo wa kutosha wa kuongozza Umma na vyombo vyake, ili kutekeleza majukumu yake ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake.

**(5) Kujikosoa na kukosoana ni silaha ya Mapinduzi**

58. Kuna mambo mawili tuliyojifunza ambayo ni muhimu pia kuyazingatia. La kwanza linahusu suala la kukosoa, kujikosoa na kukosoana kama njia ya kukijenga na kukiimarisha Chama na wanachama. Ni kweli kuwa katika TUJISAHIHISHE Mwalimu anasisitiza jambo hili na kwamba Katiba ya CCM inatamka waziwazi juu ya umuhimu wake. Lakini ni kweli pia kuwa hatujaijenga tabia hii ipasavyo. Mara nyingi tumependele akuteteana, kufichiana makosa na hata kutafuta visingizio visivyo na msingi. Neno kuleana, kwetu sisi (ingawa kuna malezi mema na mabaya) limechukua nafasi ya kukosoana. Wanachama wenye upungufu husaidiwa kama wanakosolewa ili wajirekebishe. Lakini hatua za nidhamu wakati mwingine zimechukuliwa bila ya mhusika kuelezwa wazi wazi upungufu wake ili ajirekebishe na pia wananchi wameachiwa wabuni wenyewe sababu.

59. Suala la kukosoa, kujikosoa na kukosoana lina sura kadhaa. Kwanza linataka wanachama na viongozi kuwa tayari kusema kweli katika vitendo vyao na kukubali kuambizana ukweli. Pili, linataka wanachama na hasa viongozi wawe tayari kukosolewa bila kuhamaki na inapobidi kukubali kujirekebisha. Tatu ni kuwa Chama chenyewe katika vikao vyake vya ngazi mbalimbali kuwa na utaratibu wa kujikosoa.

60. Sura hii ya tatu ni muhimu sana kwa mafanikio ya utekelezaji wa siasa ya hama. Kuongoza ni kutoa maamuzi yanayohusu utekelezaji wa siasa. Kujikosoa kama Chama ni kuwa na utaratibu wa kuyarudia maamuzi ya nyuma, kuona jinsi yalivyotekelezwa na kupima matokeoa ya utekelezaji huo kwa kuzingatia nia ya Chama katika kutoa uamuzi huo. Kama makosa yamefanyuika katika utekelezaji basi ni muhimu kutafuta sababu za makosa hayo na kuchukua hatua za haraka za kuyarekebisha. Makosa pia yanaweza kutokana na uamuzi wenye kutokuwa sahihi. Katika hali hiyo, itabidi uchambuzi ufanywe ili kubainisha kiini cha upungufu wa uamuzi huo na kuchukua hatua za kurekebisha mambo. Kama kuna mafanikio basi ni nafasi kwa Chama kuzingatia mbinu zilizotumika kwa manufaa ya utekelezaji wa baadaye. Hivyo utaratibu wa kujikosoa kwa Chama ukiteelezwa kwa dhati ni shule kubwa ya ujenzi wa Ujmaa.

61. Ni dhahiri kuwa mapinduzi yetu yangakuwa yamepiga hatua kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa kama TUNGEZINGATIA UTARATIBU HUU WA HARAKATI ZA KUJENGA UJAMAA. Mfano mmoja unatosha kuelezea ukweli wa mambo. Msimamo wa Chama juu ya UJAMAA VIJIJINI uliopitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama, Mwanza, mwezi Oktoba, 1967. Tangu wakati huo wananchi wameitikia mwito huo kwa njia na mafanikio mbalimbali. Lakini hadi sasa, miaka kumi na minne baadaye, hakuna kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa kilichokaa na kupima maendeleo ya Ujamaa vijijini, kubainisha kilichofanya kuwa mpaka sasa sekta ya ujamaa vijijini ikawa bado finyu na kutafuta malengo na mbinu mpya za kuleta msukumo wa ujenzi wa ujamaa vijijni. Ni dhahiri kuwa Chama kingalifanya hivyo kila mwaka na baada ya kila miaka mitano, kiwango cha ujamaa vijijini na nchini kingelikuwa cha juu kuliko kilivyo sasa na kwamba Chama kingalikuwa na hasina kubwa zaidi ya mbinu za kuongoza harakati za ujamaa. Na kwa kuwa ujamaa vijijini kwanza kabisa ni utengenezaji mali, basi maendeleo ya vijijini hii leo yangekuwa yameopiga hatua kubwa na kwamba huenda matatizo ya sasa ya upungufu wa ziada ya mazao nchini yangelikuwa yamepatiwa ufumbuzi wake.

62. Msimamo wa kujikosoa ni msimamo wa kimapinduzi. Unazingatia upungufu wa binadamu na papo hapo kutambua uwezo wa binadamu wa kufanya vizuri na zaidi mradi tu anajipa nafasi ya kujifunza. Kujirekebisha na kujaribu tena na tena. Kwa Chama cha kijamaa kama Chama cha mapinduzi hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya kujikosoa.

**Umuhimu wa kuzungumzia jinsi ya kutekeleza**

63. Jambo la pili tulilojifunza katika kujikosoa na ambalo linahitaji kuzingatiwa linahusu methodolojia ya kuunganisha uamuzi wetu na utekelezaji. Tumekuwa na tabia ya kuzungumzia suala na kufanya uamuzi. Baada ya hapo tunaachia utekelezaji ufanyike kwa kutegemea hisia, uwezo na msimamo wa wanaohusika. Kwa kawaida, suala la kuzungumzia namna ya kutekeleza, kuzungumzia mipango na mbinu za utekelezaji, hatukuwana tabia ya kulishughulikia hasa kitaifa. Huu ni upungufu katika Chama maana namna ya kutekeleza uamuzi, mipango na mbinu za utekelezaji ni sehemu muhimu ya harakati za kutafsiri fikra (uamuzi katika vitendo na ndiyo njia iliyo wazi ya kuhakikisha mafanikio ya utekelezaji.

64. Tabia ya kutozungumzia namna ya kutekeleza mipango na mbinu za utekelezaji husabaibsha matatizo katika Chama. Tatizo lililo dhahiri ni kuwa viongozi mmoja mmoja au vikao vya mikoa, wilaya na vijiji vinaachiwa vibuni njia za utekelezaji kwa kutegemea aonavyo kiongozi mhusika au kikao kihusika. Pale ambapo kiongozi mhusika ana msimamo thabiti wa chama au wajumbe wa kikao ni watu makini na wenye uwezo na busara, utekelezaji unaweza kufanyika vizuri. Lakini kuna pia sehemu nyingine katika nchi yetu na kwa vipindi mbalimbali ambako viongozi wamelazimisha utekelezaji kinyume cha matazamio ya Chama na wananchi na mara nyingine hata kusababisha usumbufu usio wa lazima kwa wananchi. Ufafanuzi wa namna ya kutenda na mbinu za utekelezaji unajenga nidhamu katika utekelezaji, unarahisisha usimamizi wa shughuli za Chama katika ngazi zote na unajenga nidhamu katika utekelezaji unarahisisha usimamizi wa shughuli za Chama katika ngazi zote na unawezesha kutumika kwa utaratibu wa kujikosoa na kukosoana. Zaidi ya hayo, unaimarisha umoja na nguvu za Chama

kama chombo cha kutenda, yaani kuongoza mapinduzi ya kujenga Ujamaa Tanzania.

65. Mwongozo mpaka hapa umegusia historia ya mapambano ya taifa letu katika vipindimbalimbali, umechambua mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kutekeleza siasa ya Chama ya ujamaa na kujitegemea na kumalizia kwa kufanya uchambuzi wa kujikosoa katika Chama ili kwa kuzielewa nguvu na upungufu wa Chama chetu tuweze kujizatiti kwa kuikabili kati kubwa iliyo mbele yetu.

66. Historia ya nhi yetu tangu kuzaliwa kwa TANU na ASP ni historia ya mapambano makali dhidi ya ukoloni na ubeberu na tumfanikiwa kupata ushindi mwaka hadi mwaka. Hali yetu ya uchumi na ya jamii ni ngumu kuloko ambavyo imewahi kuwa tangu tupate uhuru. Uko nyuma tulishinda katika mapambano yetu kutokana na umoja wetu wa kitaifa, usahihi wa siasa yetu na uongozi bora wa Chama. Leo na katika siku za usoni tutahitaji umoja imara zaidi, siasa sahihi na uongozi bora wa chama. Lakini katika kipindi hiki ambapo ubepari na ubeberu wa dunia umejitokeza hadharani kwa kampeni na njama za kuhudumu ujamaa na kutaka kulibana Taifa, wakati ambapo vibepari na vibwanyenye vya humu nchini vimeonyesha dhahiri uhasama wao dhidi ya maslahi ya wakulima na wafanyakazi, umoja wa sasa lazima usimame juu ya misingi iliyo wazi na sahihi, misingi ya ujamaa; kwa hiyo ni umoja wa wakulima na wafanyakazi na wale wote wanaounga mkono kwa vitendao ujenzi wa ujamaa nchini.

# SEHEMU YA TATU

## KUJENGA MSINGI WA UCHUMI WA UJAMAA NA TAIFA LINALOJITEGEMEA

67. Lengo kuu la mapinduzi ya Tanzania ni kujenga nchi ya ujamaa ambamo unyonyaji wa mtu na mtu utakuwa umetokemezwa, ambamo uchumi wa taifa utakuwa unamilikiwa na kudhibitiwa na umma wa wakulina na wafanyakazi washiriki na ambamo uhusiano wa watu katika jamii utakuiwa ni wa udugu na kushirikiana kwa maendeleo ya wote na ambamo kati imepewa hadhi ya kuwa wajibu wa kila mtu.

68. Uamuzi wa kujenga ujamaa Tanzania ni uamuzi wa kimsingi na kuhistoria na haubadiliki. Chama kilijua tangu mwanzao kuwa kujenga ujamaa hakungekuwa mteremko bali ni mapambano magumu dhidi ya ubepari na unyonge wa humu humu ndani na dhidi ya njama za ubeberu wa dunia. Na isitoshe, Chama kilijua tangu mwanzo kuwa kujenga ujamaa wenyewe katika ubinafsi na upungufu wetu wa aina mbalimbali. HaRAKATI ZA MIAKA KUMI NA MINNE TANGU Azimio la Arusha zimetuthibitishia ukweli huu.

69. Mapambano ya kutekeleza siasa ya ujamaa ya Chama katika miaka kumi na mnne tangu Azimio la Arusha yametuwezesha kufanya mabadiliko ya kimsingi katika uchumi wa nchi yetu. Kabla ya Azimio la Arusha uchumi wetu ulikuwa na mfumo wa kikoloni mamboleo kwani benki, bima, biashara ya nje yote yalikuwa matawi tu ya makampuni ya kibepari ya ulaya na marekanai wakati mazao ya kilimo cha biashara yaliwekewa lento la kutumikia viwanda vya kibepari vya nchi za ng'ambo.

70. Kutaifishwa kwa benki, bima na kampuni za biashara za nje za kibepari na kuanzishwa kwa mashirika ya biashara ya ndani na ya nje katika kutekeleza Azimio la Arusha kumeleta marekebisho ya kimapinduzi ya mfumo wa uchumi. Hatua thabiti zimechukuliwa pia za kuanzisha na kupanua viwanda vinavyotumia

bidhaa asili za kilimo chetu kama ngozi, pamba, katani, korosho, tumbaku, pareto, miwa miwa na kadhalika. Kwa upande wa kilimo hatua za mwanzo zimechukuliwa kukielekeza kwenye mfumo wa kijamaa: sehemu kubwa ya mashamba ya kibepari, hasa ya mkonge ilitaifishwa, mashamba makubwa kadhaa ya Taifa ya kilimo na ya ufugaji yameanzishwa wakati sekta ya ujamaa katika baadhi ya vijiji imeanza kushanmiri. Tanzania Visiwani, Serikali ya Mapinduzi ilitaifisha ardhi, benki, nyumba na kuanzisha mashirika ya biashara ya nje na ya ndani na kuanzisha viwanda vinavyotumia miwa na mbata. Hatua zote hizi zilichukuliwa zimetujengea msingi wa uchumi wenye mwelekeo wa nchi ya ujamaa. Mafanikio haya yamewezekana kutokana na kazi, ujasiri na kujitolea mhanga kwa wakulima na wafanyakazi chini ya uongozi wa Chama.

71. Lakini, pamoja na mafanikio haya, cnhi yetu hivi sana imekubwa na hali mbaya ya uchumi kama vile hali hiyo ilivyozikumba nchi zote duniani, zilizoendelea na zisizoendelea, nchi kubwa na ndogo, za kibepari na za kijamaa. Hali hii lazima tuikabili kwa kujipa kazi mbili ambazo zitakwenda sambamba. Kazi moja ni kutekelez malengo ya muda mrefu yakujenga msingi wa uchumi wa kijamaa wa taifa linalojitegemea. Na kazi ya pili ni kuchukua hatua thabiti kuanzia sasa za kujihami kiuchumi ili kuhakikisha kuwa hali ya uchumi wetu haiendelei kudidimia na kuathiri hata msingi tuliokwisha ujenga.

72. Ni muhimu kutamka hapa kuwa siasa ya uchumi ya Chama cha Mapinduzi ina lengo la kutosheleza mahitaji ya wananchi ya chakula na kulipa Taifa uwezo wa kujitegemea katika mahitaji ya maendeleo ya sasa na ya baadaye.

## MWELEKEO WA MAENDELEO YA UCHUMI NA JAMII YA MUDA MREFU

73. Chama Cha mapinduzi kiimekwishatoa mwelekeo wa maendeleo ya uchumi na jamii kwa miaka ishirini ijayo. MWONGOZO wa Chama unayazingatia hayo ndiyo msingi wa mwelekeo wake wa uchumi na wa jamii kwa kipindi hicho.

74. Kwa hiyo, Mwongozo wa Chama hautayakariri yaliyomo katika mwelekeo wa maika ishirini isipokuwa kusisitiza juu ya masuala yanayohitaji mkazo maalum na pia kutoa mwelekeo mpya pale ambapo pana umuhimu wa kutazamwa upya na hapakushughulikiwa na mwelekeo wa maendeleo ya miaka ishirini.

75. Mambo makubwa mawili yanastahili kutajwa katika kiwango hiki. La kwanza linahusu kilimo. Kwa kuwa kilimo ndio msingi wa maendeleo yetu ya sasa na ya miaka mingi ijayo, ni muhimu kwa Chama kulitilia mkazo suala hili kwa kufanya ufafanuzi wa nafasi ya kilimo katika maendeleo ya uchumi wa taifa na njia inayohitajika kuhudumia maendeleo hayo. Hivyo, suala la kilimo na hasa kilimo cha kijamaa linapewa nafasi kubwa katika mwongozo huu.

76. Jambo la pili linahusu mfumo wa upangaji wetu wa maendeleo. Kwa kuzingatia kwamba maendeleo ya kijamaa ni maendeleo yaliyopangwa Chama katika kipindi kinachoanza sasa kitalitazama kwa undani zaidi suala la upangaji wetu wa mipango ya maendeleo kwa madhumuni ya kuimaisha na kukaza usimamizi wa utekelezaji. Chama kitaona kama Tume ya Mipango katika sura yake ya sasa kinatimiza makusudio ya Chama. Wakakti huo huo Tume ya Bei itafanyiwa uchambuzi ili ipatiwe nafasi yake ya kuwa chombo cha upangaji wa uchumi badala ya kuwa chombo cha biashara kama ilivyo sasa. Sifa moja kubwa ya uchumi wa kijamaa ni kwa ni uchumi wa mpango tofauti na uchumi wa kibepari ambao ni uchumi wa soko . Uchumi wetu kwa sasa ni mchanganyiko: kwa sehemu fulani unapangwa na kwa sehemu kubwa unatemea mvutana wa soko. Chama kitalitazama suala hili kwa undani zaidi ili kuelekeza zaidi uchumi wetu kwenye mfumo wa uchumi wa mpango kuliko ilivyo sasa. Nafasi ya Tume ya Mipango na Bunmge katika kupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango itatazamwa upya. Aidha, matumizi ya fedha za kigeni yataingizwa katika mfumo wa upangaji mipango.

77. Kwa kuwa uchumi wa kijamaa ni uchumi wa mipango, basi tutahitaji watu wenye taaluma ya kupanga katika taifa. Mikoa , Wilaya na Vijiji na kwa viwango mbalimbali vya utaalamu. Hivyo Serikali itawajibika kuwaandaa mapema iwezekanavyo wataalam wa mipango kwa wingi. Wakati huo huo ihakikishwe

kuwa upangaji wa kinchi unapewa uzito sawa na upangaji wa kimradi ambao ndio unaoeleweka zaidi wa wataalam wetu.

## A. MAPINDUZI KATIKA KILIMO NDIYO KAZI YA UMUHIMU WA KWANZA

78. Msingi wa uchumi wa nchi yetu ni kilimo. Asilimia themanini na tano ya Wanzanit wanaishi kwa kilimo; biashara yetu na nchi za kigeni inategemea zaidi mazao tunayoyatoa katika kilimo, viwanda vichache tulivyonavyo nchini vinategemea mazao ya kilimo uwezekano wa kutoa ziada itakayowezesha nchi kugharimia mapinduzi ya viwanda (kugharimia viwanda vya madawa) upo katika sekta ya Kilimo.

79. Katika hali hii, uongozi na usimamizi thabiti na makini wa Chama cha Mapinduzi uelekezwe zaidi katika sekta hii ya uchumi wa Taifa. Kazi iliyo mbele yetu ni kuleta mapinduzi katika kilimo. Kwa kuwa asilimia themeanini na tano ya Watanzania ni wakulima wa vijijini, basi mkazo wa mapinduzi katika kilimo lazima uwe kilimo cha vijijini wakati mashamba ya Taifa pia yanashughulikwa.

80. Mapinduzi ya kilimo vijijini katika nch yetu ni kilimo cha kiamaa na cha kisasa ambacho kina sifa zifuatazo: Kwanza ni kilimo cha mashamba makubwa ya kijamaa ya vijiji, pili ni kilimo kinachotumia pembejeo, zana za utaalamu na tatu ni kilimo kinachotekelezwa kwa utaratibu bora wa kazi unaoleta ufanisi.

81. Sifa moja ya kilimo cha kisasa duniani kote ni kwa ni kilimo cha mashamba makubwa. Tofauti iliyopo ya mashamba hayo ni katika umilikaji. Katika nchi za kibepari mashamba hayo makubwa ni mali ya mabepari, wakati katika nchi za kijamaa mashamba hayo makubwa ni mali ya Taifa au ni mali ya ushirika wa wanavijiji. Hali hiyo imeanza kujitokeza pia katika kilimo cha kisasa mchini Tanzania.

82. Mantiki iliyokisukuma kilimo cha kibepari cha kisasa kiwe cha mashamba makubwa ni ile ile iliyokisukuma kilimo cha kijamaa cha kisasa kiwq cha

mashamba makubwa.  Kilimo cha kisasa ni kilimo cha zana na ukishavuka  kilimo cha plau za maksai na kuingi a katika matrekta na mashine nyingine za kupandia na kuvunia, basi ni hasara kubwa kuzitumia zana hizo katika vishamba vidogo vidogo vya ekari kadhaa tu.  Ufanisi wa hali ya juu unapatikana wakati zana hizo zinatumika katika maeneo makubwa.  Wakati  huo huo ni kuwa zana hizi za kisasa ni aghali na haiwezekani kwa kila mkulima mwenye ekari chache kupata uwezo wa kuzinunua hata katika nchi  za kibepari.  Hivyo, katika nchi za kibepari ni wakulima wakubwa tu ndio wenye uwezo wa kumiliki zana hizi na katika mashindao hayo, wakulima wadogo wamelazimika kutoa nafasi wa wakulima wakubwa,  Katika nchi za kijamaa uwezekano wa kumiliki zana hizi ni kwa kupitia Serikali (Mashamba  ya Taifa) na ushirika wa wakulima vijijini.

83. Uwezekano wa kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya ujamaa vijijini ni mkubwa   katika Tanzania maana mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa katika vijiji vilivyotekeleza ujamaa vijijini yameufungua macho umma wa Wakulima vijijini.  Wakati huo huo maeneo ya kuanzisha na kupanua mashamba ya ujamaa hayana matatizo katika sehemu kubwa ya vijiji vyetu  nchini mradi tu kuna nia, mipango na uongozi thabiti.

84. Wakulima vijijini wamepiga hatua za mwanzao katika kutekeleza maagizo ya Siasa ni Kilimo kwa upande wa masharti ya kilimo bora cha mazao ya chakula na mazao ya biashara.  Pembejeo za viwanda na samadi zimeanza kutumika pia. Katika siku za usoni Chama kitawajibika kufanya mambo mawili kuendelea kuwaelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kutimiza masharti ya kilimo bora na kuhakikisha kuwa serikali inakuwa na mipango thabiti ya upatikanaji wa pembejeo na kwa bei nafuu kwa wakulima.  Matumizi ya samadi lazima yahimizwe kwa mkazo zaidi.

85. Suala la zana za kisasa ni gumu zaidi.  Hivi sasa sehemu kubwa ya kilimo vijijiniinalimwa kwa jembe la mkono.  Kuna maeneo yenye mifupa mingi ambako kazi ya kilimo inaendeshwa pia na plau za kubutwa na maksai.  Yapo  pia matrekta katika baadhi ya vijiji. Lengo la Chama katika miaka ijayo ni kumtoa mkulima kutoka kwenye hali yake ya sasa ya kutegemea jembe la mkono na

kumfikisha kwenye kutumia zana za kisasa. Kazi hiyo, pamoja na ya kuhakikisha kuwa matumizi ya mikokoteni yanaenea vijijini kote lazima itekelezwe kwa nguvu zote.

86. Wakati huo huo Chama kihakikishe kuwa serikali inaagiza matrekta toka ng'ambo kwa kuzingatia uwezo na uzito unaolingana na umuhimu wa kilimo kwa maendeleo ya Taifa letu. Kupanga ni kuchagua. Hivyo, kama kwa mfano, ni kuchagua kati ya magari madogo na matrecta, basi uzito uwe kwenye matrekta. Lakini, kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wetu (upungufu wa fedha za kigeni na kwamba hatuna viwanda vyetu vya chuma na vya matrekta), itachukua muda wa miaka mingi kabla ya kilimo cha trekta kuwa ndicho kilimo cha vijiji vyetu. Kwa sasa mbinu ya kutufikisha huko siyo kungoja matrekta bali ni kutumia majembe ya mkono na plau za maksai katika kilimo cha kijamaa na cha binafsi vijijini ili kuongeza ziada ya mazao kitaifa ambayo ndiyo ufunguo wa kulipatia Taifa uwezo wa matrekta zaidi na kukuza uwezo wetu wa kuanzisha viwanda mama na vinginevyo>

87. Sifa ya tatu ya mapinduzi ya kijamaa katika kilimo vijijini ni utaratibu wa kazi wenye ufanisi. Shughuli za kijamaa vijijini huko nyuma zimezoroteshwa pia kutokana na vijiji kutokuwa na utaratibu mzuri wa kazi. Mara nyingi kazi za ujamaa zimefanywa holela, bila kujali ufanisi wa kuridhisha. Chama kitawajibika kuhakikisha kuwa unabuniwa utaratibu wa kupanga na kugawa kazi kwa mfumo ambao utajenga nidhamu, kurahisisha utekelezaji wa majukumu, kubainisha mchango wa kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi kuendeleza hisia za ushirikiano na kuongeza ufanisi.

88. Lakini mapinduzi katika kilimo nchini lazima pia yaambatane na mapinduzi ya msimamo wa serikali na vyombo vyake kuhusu nafasi ya kilimo katika mapambano ya ujenzi wa taifa. Katika siku za usoni, hama kitahakikisha kuwa serikali na vyombo vyake, kwa vitendo, vinautekeleza wajibu wake wa kuhudumia na kusukuma maendeleo ya kilimo, kilimo cha kijamaa kikipewa nafasi ya kwanza.

89. Mapinduzi katika msimamo ni pamoja na kuupiga vita umangi meza na mila na tabia zinazopingana na mahitaji ya kilimo cha kisasa na pia kubuni njia bora zaidi za kuandaa wataalamu watakaohitajika sana vijijini kama zile zilizotuwezesha kutekeleza Azimio la Musoma kuhusu Elimu ya msingi kwa wote. Kwa kuwa kilimo cha kijamaa ni kilimi cha mashamba makubwa, basi ihakikishwe kuwa mafunzo ya kilimo yanazingatia pia suala la menejimenti ya mashamba makubwa.

## B. HATUA NYINGINE ZA UMUHIMU WA KWANZA KATIKA UCHUMI

90. Pamoja na maelekezo ya maendeleo ya miaka ishirini yaliyokwishapatishwa na Chama, masuala yafuatayo yanahitaji kusisitizwa:

### (1) **Kilimo cha umwagiliaji maji**

91. Kilimo hiki kimepewa umuhimu wake katika mwelekeo wa muda mrefu. Kwa kuelewa kuwa pamoja na miradi mikubwa ya kitaifa ya umwagiliaji, miradi midogo midogo ya vijijini ndiyo ambayo inaweza kutoa matunda ya haraka,hatua za dhati zichukuliwe za kuandaa wataalam wa fani hiyo kwa wingi nchini na ng'ambo na pia kutafuta uwezekano wa kuanzisha kiwanda cha zana za umwagiliaji maji. Wakati huo huo Chama kijizatiti barabara ili kuimudu kazi ya kuwashirikisha wananchi, maana utekelezji wa miradi ya umwagiliaji vijijini utategemea zaidi jasho la wananchi wenyewe kuliko matumizi ya zana za kisasa.

### (2) Kilimo cha matunda na mboga

Kilimo hiki hadi sasa hakijatiliwa mkazo nchini. Licha ya mahitaji ya chakula bora yanavyozidi kuongezeka, matunda na mboga yanaweza kuwa mazao muhimu ya biashara ya nje kwa nchi yetu. Nchi nyingi za Afrika ambazo hazina mazingira bora zaidi ya haya ya nchi yetu hijipatia fedha nyingi za kigeni kutokana na matunda na mboga. Chama kihakikishe kuwa miradi ya Taifa na ya vijiji ya kilimo cha matunda na mboga za kutosha nchini kote na ziasa ya

kuuza ng'ambo. Katika lengo maalum la kuwapatia wafanyakazi wa mijini matunda na mboga kwa wingi, vijiji vilivyo karibu na miji mikubwa visaidiwe kuanzisha miradi mikubwa ya vijiji ya mazao haya.

### (3) Uendelezaji wa mifugo na ufugaji

Tanzania ina utajir mkubwa wa mifugo hasa ng'ombe, mbizi na kondoo. Inakisiwa kuwa idadi ya ng'ombe peke yake waliomo nchini ni zaidi ya milioni kumi. Lakini hali ya mifugo yenyewe ni duni maana wafugaji walio wengi bado wanathamini zaidi wingi wa mifugo badala ya ubora wa mifugo. Misingi ya ufugaji wa kisasa haijafikishwa ipasavyo kwa wananchi na ina boa za mifugo kwa ajili ya maziwa na nyama hazijaenezwa nchini.

Katika hali hii kazi kubwa ya Chama katika fani ya mifugo itakuwa kuhakikisha kuwa Serikali inaandaa sera ya kuendeleza mifugo nchini na kuhakikisha kuwa wafugaji wanaelimishwa na wanatekeleza misingi ya ufuagaji wa kisasa na kuchukua hatua za dhati za kueneza mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na wa nyama.

Chama kitaongoza jitihada za kuanzisha na kupanua ufugaji wa kijamaa vijijini kwa njia ya ranchi za ng'ombe bora wa maziwa na ranchi za vijinini za kunenepesha mifugo. Katika hali hiyo, suala la mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini linakuw la umuhimu wa kwanza.

Jingine la kulikabili ni suala la uhaba wa nyama, maziwa na mayai na bei za juu mno za mazao hayo nchini. Ili kulipatia ufumbuzi tatizo hili, Chama kitawajibika kuhakikisha kuwa serikali inaingiza katika mipango yake miradi mikubwa ya ufugaji wa kuku, nguruwe na ng'ombe karibu na miji mikubwa. Aidha, Chama na Serikali visaidie vijiji vinavyozunguka miji kuanzisha miradi ya ufugaji hasa wa kuku, nguruwe, sungura na nguruwe na ng'ombe karibu na miji mikubwa. Aidha, Chama na Serikali visaidie vjiji vinavyozunguka miji kuansisha miradi ya ufugaji hasa wa kuku,

nguruwe, sungura na ng'ombe wa maziwa.

Wakati huo huo, jitihada za kueneza mifugo katika maeneo yasiyo nayo ya kutosha tabidi isimamiwe na Taifa. Pamoja na kwamba waugaji wengi wa Tanzania wana nmifugo mingi, bado wengi wao hawitumii wala kuiona mifugo kama chombo cha kuwaletea maendeleo na maisha bora zaidi. Hivyo, suala la kutumia mifugo ili kuinua hali halisi ya maisha ya wafugaji na ya vijiji vyao lazima liwe mkabala maalum wa Chaa kuanzia sasa.

### (4) Viwanda

Jambo la kusisitiza linahusu hali ya utengenezaji mali katika viwanda vilivyopo nchini hivi sasa ambapo vilivyo vingi havitengenezi malikwa kadiri ya uwezo vilivyo nao. Chama itabidi kijihusishe na matatizo ya viwanda hivi na kuhakikisha kuwa vinapata misaada yote ili viweze kutengneza mali kwa kadiri ya uwezo wake. Licha ya matatizo ya vipuri na utaalam, viwanda hivi vinakabiliwa pia na matatizo ya kisiasa kama vile upungufu wa mwamko wa siasa na utovu wa nidhamu.

Viwanda vingi tulivyonavyo nchini hutoa makapi ambayo yangeweza kutumika kwa utengenezaji wa bidhaa nyingine, lakini jitihada hiyo haijafanywa. Viwanda kama vya sukari, mafuta, mboleo, nyama na vya aina hiyo. Kuanzia sasa Serikali itawajibika kuandaa mipango ya kuyatumia makapi yatokanayo na viwanda vya aina hiyo ili kutengeneza bidhaa zinazoweza kutengnezwa.

Chama pia kitatilia mkazo utekelezaji wa Agizo la Viwanda Vidogo Vidogo mijini na vijijini. Cha,a kitahakikisha kuwa kila Mkoa unaandaa mpango wa muda mrefu wa utekelezaji wa Agizo hili la viwanda vidogo.

### (5) Mwamko wa Siasa wa wafanyakazi

Mwanko wa siasa una uwezo mkubwa wa kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuwatia wafanyakazi ari na makini zaidi katika kazi. Hali ya sasa

viwandani na ofisini inaonyesha upungufu wa mwamko wa siasa. Hisia za kimapinduzi za kuthamini kazi na wajibu, moyo wa uaminifu na wa kujitoea muhanga, tabia ya kuthamini mali ya umma, yote haya yamepotez nguvu zake.

Ni jukumu la Chama kutia pumzi mpya wakati wote katika viwanda, Serikalini na katika Mashirika ya Umma itakayoleta vuguvugu la kimapinduzi miongoni mwa wafanyakazi kwa kuuinua mwamko wao wa siasa, mwamko wa uvumbuzi, ili waongeze juhudi ya kazi wakitambua kuwa sehemu zao za kazi ndio uwanja wao wa mapambano ya kujenga ujamaa na hivyo washiriki kwa dhati katika harakati hizo.

### (6) Wizi wa mali ya umma, hujuma katika uchumi, magendo na ujambazi

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu wa aina mbalimbali nchini tangu tupate uhuru. Uhalifu wenye kutia wasiwasi maalum ni uhalifu katika uchumi. Wizi wa mali ya umma umeanza kuwa jambo la kawaida. Kumekuwa na matukio ya baadhi ya maafisa kuhusika na kuidhinisha mikataba na kampuni za nchi za nje bila kujali maslahi ya Taifa. Wakati huo huo vipusa, dhahabu na na mali mbalimbali z taifa zinatoroshwa nje ya nchi kwa magendo na kusabisha hasara kubwa kwa Taifa. Ujambazi wa kutumia silaha nao umetumika ili kunyang'anya mali na kutisha wananchi.

Chama kitahakikisha kuwa serikali inachijua hatua kali za kupambana na vitendo hivi vinavyodhoofisha uchumi wa Taifa. Iko haja pia kwa sasa ya kubuni sheria maalum zitakazoelekezwa kwenye vita dhidi ya uhalifu katika uchumi unaozidi kuongezeka.

**(7) uharibifu wa vyonmbo vya kazi na wa mali ya uuma:**

Imezuka tabia ya aibu nchini ambayo imekuwa ikiongezeka ya vitendo vya kuharibu na kuvitumia vibaya vyombo muhimu vya kazi na mali ya umma kwa jumla. Magari, matrekta zana nyingine muhimu za Chama, Serikali na Mashirika ya Umma mara ningi hayadumu muda mrefu kama ambavyo ingetazamiwa kutokana na matumizi mabaya. Nchi inapatishwa hasara kubwa ya fedha za kigeni itokanayo na ajali za malori, mabasi, magari madogo n.k. zinazosababishwa na uzembe na ulevi. Kuna tabia ya baadhi ya abiria kuharibu mabehewa ya treni ambayo kesho watahitaji kuyatumia mabehewa hayo hayo tena. Tunalo tatizo vile vile la tabia ya kuchaua na kuharibu nyumba za serikali na za mashirika za kuishi inayofanywa na baadhi ya wapangaji wenyewe. Wakati mwingine majengo ya ofisi za chama, Serikali na Mashirika ya Umma hayahifadhiwi na kuhuddumiwa ipasavyo.

Tabia ambayo baadhi ya mifano yake imetolewa hapo juu ni ishar kuwa na kuna mushkeli wa msimamo katika jamii. Chama kuanzia sasa kitalifanyia uchunguzi suala hili ili kukielewa chanzo chake na kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

## MAENDELEO YA JAMII

92. Katika kipindi kichachoanzia sasa chama kitatilia mkazo suala la ujenzi wa tabia na maadili ya kijamaa nchini. Pamoja na jitihada iliyofanywa ya kutoa elimu na kuunda vyombo vya umma, jamii yetu bado inazo mila, tabia na maadili yaliyo kinyume na maadili ambayo yanafanana na misingi ya siasa ya ujamaa tunayosukudia kuijenga.

93. Watu wameanza kuthamini zaidi vitu kuliko utu na tamaa ya kujipatia mali bila ya kuitokea jasho inaenea, matukio ya wizi wa mali ya umma yameongezeka. Lakini lililo baya zaidi ni kuwa mwizi wa aina hiyo anapogunduliwa, baadhi ya wananchi badala ya kumfichua au kulaani kitendo chake, humsifu na

kumhusudu. Wakakti mwingine mvivu na mtegaji kazini hutetewa hata na vyombo vya Chama vyenyewe. Wakati huo huo, bado kuna mabaki ya tabia ya kupuuza elimu ya shule kwa watoto na badala yake kuna wazazi wanaopendelea watoto wao wachungaji mifugo au hata kuolewa badala ya kuendelea na shule.

94. Jitihada ya Chama za kujenga tabia na maadili ya kijamii itaelekezwa kwenye taasisi muhimu za nchi kama shule na vyuo, majeshi na sehemu za kazi. Lakini Chama kitahakikisha pia kuwa maisha ya hadhara ya jamii yetu yanasaidia kujenga misingi ya tabia na maadili ya Taifa linalojenga ujamaa na la kimaendeleo kwa ujumla. Hivyo, Chama kitapiga vita tabia ya baadhi ya wananchi na hasa wakiwa viongozi inayokwaza na kupotosha umma. Jamii lazima iwe shule ya kwanza ya maadili ya kijamaa.

**(1) Maendeleo ya jamii:**

(a) Uchumi wa fdha ni mpya katika nchi yetu na ndiyo maana tabia ya kutumia fedha kwa mipango haijaenea. Chama kitaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutumia fedha kwa mipango, kuweka akiba benki na kupiga vita tabia ya ufujaji mali na matumizi ya fahari.

(b) Uzururaji wa aina mbalimbali umeongezeka nchini. Ka kuzingatia kushindwa kwa hatua za pupa zilizotumika katika siku za nyuma, Chama kitalitafakari kwa undani zaidi suala la mipango na mbinu za kupambana na uzururaji kwa kutia maanani kuwa ufumbuzi wa kudumu utategemea maendeleo ya ujenzi wa ujamaa vijijini pamoja na mipango thabiti ya kuwa shirikisha wakati wa mijini katika ushirika wa viwanda vidogo. Vijiji ambavyo vimepiga hatua za ujamaa vimekwishaanza kulitatua tatizo la uzururaji na vimeanza kuwa na mipango ya kuwatunza vikongwe na walemavu.

(c) Utaratibu wa bima na pensheni hauwezi kuwa na wafanyakazi pekee. Katika siku za usoni Chama kitahakikisha kuwa unaanzishwa utaratibu wa

bima na pensheni kwa wakulima washirika kwa kutegemea maendeleo yao.

(d) Haji ya vijiji vingi ingali duni kwa ustawi wa jamii na utamaduni. Chama kitalishughulikia suala la kuleta mapinduzi ya mazingira vijijini katika fani hiyo.

(e) Kuhusuwalemavu, Chama kitahimiza serikali kuchukua hatua za kuimarisha na kuvipanua vifaa muhimu kwa walemavu kama baiskeli, viatu, magongo, na kadhalika.

**(2) Elimu:**

Chama kuanzia sasa kitajihusisha zaidi na shughuli za elimu nchini hasa kwa upande wa maandalizi ya waalimu na maendeleo yao na ya shule na vyuo maana waalimu wana mchango mkubwa wa kutoa katika kumjenga Mtanzania mpya. Katika lengo hilo, Chama kitafanya tathmini ya mafanikio tuliyoyapata katika kuielewa na kuitekeleza falsafa ya Chama ya Elimu ya Kujitegemea.

Aidha, Chama kitalitazama upya Agizo la musoma katika vipengele vyake vyote. Kwa sasa imedhihirika kuwa utekelezaji wa Azimio hilo kuhusu utaatibu wa kuingia Chuo Kikuu unahitaji mabadiliko ya msingi.

Pamoja na mafanikio tuliyopata katika Elimu ya Watu wazima Chama kitaendelea kuhimiza wananchi na hasa wanaCCM na viongozi kujiendeleza kwa elimu kwa kadiri ya uwezo wao na kujenga tabia ya kusoma kama sehemu ya maisha yetu.

**(3) Afya:**

Kazi moja muhimu ambayo ni ya Chama katika miaka ijayo ni kuhimiza kuenezwa kwa elimu ya kinga ya maradhi pamoja na kuongoza mapambano dhidi ya tabia na mila zisizo nadhifu. Hali ya afya ya wananchi wengi vijijini inaathiriwa na tabia na mila ambazo zinapingana na maendeleo ya jamii kama vile tabia ya

kutotumia vitanda, tabia ya kuishi katika nyumba moja na mifugo, tabia ya kutotumia vyoo, tabia ya kunywa maji yasiyochemshwa, miiko mbalimbali,na kadhalika. Wakati huo huo Chama kitatilia mkazo suala la usafi wa mazingira mijini vijijini pamoja na umuhimu wa kuwepo kwa vyoo vya umma mijini.

**(4) Ujenzi wa nyumba:**

Mahitaji ya ujenzi wa nyumba za kuishi mijini na wa majengo ya ofisi na viwanda nchini yanazidi kuwa makubwa. Kazi moa ya Chama ni kuona kama kuna umuhimu wa kuingiza teknolojia mpya ya ujenzi nchini itakayosaidia kutoa msukumo wa shughuli za ujenzi wa nyumba za kuishi na za kazi. Kuna ukweli kuwa upungufu wa vifaa vya ujenzi umechelewesha maendeleo ya ujenzi nchini. Lakini huenda ikadhirika pia kuwa mashirika ya Msajili wa Majumba na Shirika la Nyumba yatahitaji pia technolojia bora zaidi ili kuweza kutatua matatizo ya nyyumba za wafanyakazi mijini. Sera ya nyumba itashughulikiwa pia katika kipindi kinachoanza sasa.

**(5) Nishati:**

Suala la nishati ni la msingi kwa maendeleo ya Taifa letu. Pamoja na kuendelea kutafuta mafuta, Chama kitahakikisha kuwa serikali inazidisha mipango thabiti itakayoliwezesha Taifa kuanza kutumia nguvu za maji, makaa, upepo na jua. Pamoja na miradi mikubwa ya nguvu za maji kuna haja ya kutia maanani miradi midogo midogo ya nguvu za maji. Suala la kuni itabidi lipewe umuhimu mkubwa kwa kuwa na mipango kamambe ya kupanda miti vijijini na miradi ya Mikoa na Taifa. Chama kiihimize Serikali kuendelea na kutafuta mbinu za kutumia makaa ya mawe tuliyonayo kusukuma uchumi wetu. Umuhimu wa suala la nishati utahitaji sera maalum.

### (6) Msimamo juu ya kuendelea sayansi na teknolojia:

Mpango wa miaka Ishirini unatoa mwelekeo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, kwani sayansi na teknolojia ni msingi muhimu kwa maendeleo ya kisasa. Chama kijihusishe zaidi na mipango ya kuwapata wanasayansi na wanateknolojia wenye uwezo wa viwango mbalimbali vyautaalamu na msimamo sahihi wa siasa. Wakati huo huo, Chama kishughulikie ustawi wa wataalamu na mabingwa tulionao hivi sasa nchini ili kuhakikisha kuwa wanaishi katika mazingira yanayowawezesha kutoa mchango wao kwa ukamilifu katika ujenzi wa Taifa letu. Kutokana na kukosa msimamo sahihi wa kuwashughulikia wataalamu wetu kumewafanya baadhi ya wataalam kubabaika na Serikali kupoteza mabingwa katika fani za uganga, uhandisi, urubani wa ndege na kadhalika.

Maendeleo ya uchumi wetu hasa kwa upande wa viwanda na nishati utahitaji mafundi wa viwango mbalimbali kwa wingi sana. Chama kihakikishe kuwa serikali inakuwa na mipango thabiti ya namna ya kuwapata mafundi hawa na kwamba inatumia nafasi zinazoweza kupatikana kuwaandaa hapa nchini na ng'ambo.

95. Chama kitakuwa na utaratibu wa kuandaa mikutano na wataalamu w fani mbalimbali ili kubadilishana mawazo juu ya mbinu za kusukuma mbele mapinduzi katika sayansi na teknolojia nchini.

## D. ULINZI NA USLALAMA

*"MSINGI WA MAENDELEO Y Ulinzi na usalama wa tanzania ni Watanzania wenyewe, kila Mtanzania, na hasa kila mzalendo na kila mjamaa".*

***(Mwongozo wa TANU, 1971)***

96. Kazi kubwa ya Chama ni kuhakikisha kuwa uhuru wa taifa, mipaka ya nchi na

matunda ya uhuru na ya ujamaa ya wakulima na wafanyakazi yanalindwa na na kuhifadhiwa. Majeshi yetu yote kwa pamoja ndicho chombo kikuu cha kutekeleza siasa ya Chama ya ulinzi na usalama. Lakini chimbuko la majeshi ni Umma wa wakulima na wafanyakazi ambao pia wanashiriki katika ulinzi na usalama wa nchi yao kwa kupitia ulinzi wa mgambo na kwa kuwa macho katika sehemu zao za kazi na za kuishi viwandani na maofisini, vijijini na mijini.

97. Chama kitaendelea kuimarisha kazi ya kuyaelimisha majeshi na wananchi kwa jumla juu ya maombile ya mapambano yetu na kufanya uchambuzi wa kutambulisha maadui wa taifa na wa siasa ya ujamaa na Kujitegemea ambao ni ubepari na Ubeberu wa dunia na vibaraka wao wa humu nchini.

1. Kazi ya Chama ni kuhakikisha kuwa majeshi yetu yanakuwa tayari kwa mapigano wakato wote. Ili kufikia lengo hilo, Chama kitahakikisha kuwa wanajeshi wanakuwa na mwamko wa hali ya juu wa kizalendo na wa kijamaa na wanajengeka katika misingi ya nidhamu ya kujituma ya jeshi la kimaa. Chama kitahakikisha pia kuwa maendeleo ya teknolojia na uimarishaji wa michepuo jeshini yanapewa umuhimu wa kwanza. Ni muhimu wa Chama kuyasaidia majeshi yetu katika jitihada zao za kupambana na tabira iliyoanza kujitokeza hapa na pale majeshini ya kutothamini mali ya jeshi, ubadhirifu na tabia ya kutojali kwa jumla. Vitendo hivi ni kinyume cha ila za kijeshi na maadili ya jeshi lolote na hasa jeshi la kijamaa amayo majeshi yetu, chini ya uongozi wa Chama, yatatilia mkazo wakati wote.

2. Ushindi wetu wa vita dhidi ya majeshi ya uvamizi ya fashist Idd Amin umetudhihirishia usahihi wa siasa ya Chama ya Ulinzi na Usalama, kutuonyesha ushujaa na uzalendo wa wanajeshi wetu na uwezo mkubwa walio nao makamanda wetu wa kuongoza mapigano. Kazi ya Chama ss ni kufanya majumulisho ya ujuzi mkubwa tulioupata kwa manufaa yaharakati za ulinzi na usalama wa Taifa kwa siku za usoni. Miongoni mwa mambo yanayohitaji uchambuzi na ufafanuzi wa Chama ni uhusiano wa majeshi, nafasi ya ulinzi wa mgambo katika mfumo wa ulinzi wa usalama wa Taifa wakati wa amani na vita,

muundo wa ulinzi na usalama kwa uongozi na utendaji yaani uhusiano wa wizara na majeshi, nafasi ya wanawake katika majeshi yetu na kazi za Chama katika majeshi.

3. Chama kitahakikisha kuwa jeshi la Polisi linapata misaada yote toka Serikalini ili kuliimarisha. Jeshi la Polisi linahitaji kupewa uwezo zaidi w mafunzo ya hali ya juu ya mbinu za kupambana na majambazi na wahalifu wenye ujuzi mkubwa pamoja na kupewa uwezo wa zana muhimu za kazi.

4. Chama pia kina kazi ya kuchambua tena na kwa makini nafasi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika kusukuma mapinduzi ya ulinzi na ya uchumi wa Taifa. Pamoja na kwamba madhumuni ya awali ya J.K.T. Na J.K.U. uwezo wa kuwa chombo cha kukabili kazi za ujenzi wa barabara, majengo mabwawa n.k. kwa kwa hali ya juu zaidi, kuukuza uwezo wao wa kutoa chakula na mifugo kwa ajili ya Taifa na pia kuwezesha J.K.T. na J.K.U. kuwa mahali pa kutoa mafunzo ya muda mfupi wataalamu wengi wa kada ya chini ya ufugaji, kilimo na ufundi toka Vijijini.

5. Jambo moja tululojifunza kutokana na vita dhidi ya uvamizi ni umuhimu wa viwanda vinavyohudumia majeshi. Chama kitahimiza Serikali kulipa uzito maalum suala la kukuza na kupanua viwanda vya majeshi kwa madhununi ya kuyapatia majeshi na ulinzi na mgambo vifaa muhimu wanavyohitaji.

## E. MSUKUMO WA UJENZI WA UJAMAA

6. Imedhihirika katika kipindi cha miaka kumi na minne tangu vyombo vyake na hata baadhiya viongozi wamehusika katika kuupa nguvu na kuukuza ubepari nchini. Katika kipindi kinachoanzia sasa, Chama kitakuwa macho na kitahakikisha kuwa uwezo wea Serikali na vyombo vyake, uwezo wa Chama , unatumika kuimarisha na kuendeleza Ujamaa.

7. Katika lengo hili, dhamira ya Chama ya kujenga ujamaa ijidhihirishe kwa kuhakikisha kuwa:

(a) Benki zinaelekeza nguvu za fedha za Taifa kwenye kujenga ujamaa kwa kuvipa umuhimu wa kwanza vijiji, vyama halisi vya ushirika na mashirika ya umma.

(b) Kampuni za ummna za ujenzi zilizopo zinapewa uwezo wa kudumu kazi zaidi na kwamba kampuni mpya za umma na ujenzi zinaundwa ili kuikabili kazi ya ujenzi nchini inayoongezeka mwaka hadi mwaka. Ihakikishewe pia kuwa Serikali na mashirika ya umma hayawapi kazi za ujenzi makontrakta wa kibepari isipokuwa wakati hakuna uwezekano mwingine. Fedha za Serikali na mashirika ya umma zimesaidia sana kuupa nguvu ubepari katika sekta hii.

(c) Utaratibu wa sasa wa serikali na vyombo vyake kutumia mawakala wa biashara za nje na biashara za ndani ya nchi ukomeshwe. Utaratibu huu pia umesaidia kujenga ubepari nchini.

(d) Kamati za kugawa matrekta na magari nchini zinatoa umuhimu wa kwanza kwa mshirika na makampuni ya umma, vijiji na vikundi vya ushirika halisi.

(e) Mipango thabiti inafanywa na serikali ya kuhakikisha kuwa mtindo wa sasa wa watu binafsi kupewa zabuni za kulisha makundi ya umma kama majeshi, shule na hatua. Kwa hatua ya kwanza, vyakula vinavyoshughulikiwa na mashirika ya umma kama sembe, mchele, maharage na sukari vipatikane moja kwa moja toka huko.

(f) Usafirishaji unaofanywa na vyombo vya umma uimarishwe na kupanuliwa na kwamba ugawaji wa malori na mabasi ufanywe kwa lengo la kukuza ujamaa katika sekta hii.

(g) Kila Mkoa unaandaa mpango wa muda mrefu unaoonyesha malengo ya ukuaji wa sekta ya ujamaa katika kilimo, ufugaji, viwanda na viwanda vidogo, biashara na usafirishaji. Mpango huo uhakikishe kuwa kila kijiji viwanda vidogo; biashara na kinakuwa na malengo utengenezaji mali. Kutokana na mipango yake. Serikali iandae mpango unaoonyesha mwelekeo wa ukuaji wa sekta ya ujamaa nchini.

(h) Utekelezaji wa Siasa ya ujamaa unatilia mkazo suala la Kujitegemea maana Ujamaa unaojengwa kwa misingi ya kutemea ni ujamaa batili. Chama kitaichambua falsafa inayoongoza upangaji wetu wa mipango ili kuhakikisha kuwa mipango ijayo ya maendeleo inaonyesha waziwazi mwelekeo wa kujitegemea katika mpango. Serikali ihakikishe pia kuwa uwezo wetu wa kujitegemea katika vipuri mbalimbali unakuzwa kutumia uwezo uliopo mchini.

# SEHEMU YA NNE

## CHAMA NA MAPINDUZI YETU

*"Chama tunachokiunda tunatka kiwe chombo madhubuti katika muundo wake na hasa katika fikra zke na vitendo vyake vya kimapinduzi vya kufuatilia mbali aina zote za unyonyaji nchini, na kupambana na jaribio lolote lile la mtu kuwonea mtu, au shirika au chombo cha nchi kuonea au kudhalilisha wananchi, kudhoofisha uchumi au kuzorotesha maendeleo ya Taifa".*

**(Katiba ya CCM)**

104. Chama chetu, Chama cha Mapinduzi, ni Chama chenye historia yakipekee katika Afrika. Historia yake ni ya mafanikio na ushindi katika fani mbalimbali za utekelezaji wa malengo ya siasa yake. Wanazuoni watakapokuja andika historia ya Chama chetu wataweza kuyachambua kwa kina na mapana mafanikio hayo yasiyo na kifani.

105. Chama cha Mapinduzi ni Chama cha kijamaa. Kazi kubwa ya CCM ya sasa ni kuziunganisha nguvu zote za kijamaa na za kimaendeleo nchini na kuziongoza katika mapambano ya kujenga ujamaa Tanzania na kujenga ushirikiano wa kimapinduzi wa wajamaa na wapenda maendeleo wote katika Afrika na Dunia katika mapambano dhidi ya ukoloni, ukoloni mambo leo, ubepari na ubeberu.

106. Chama cha Mapinduzi ni chombo kikuu na cha pekee cha uongozi wa taifa letu. Kuongoza ni kuonyesha njia. Kwa hiyo, Chama chetu ni mwanga unaotumlikia njia katika hali ngumu ya mapambano ya wakulima na wafanyakazi kuelekea kwenye ujanmaa. Uhalali wa uongozi wa Chama chetu una misingi ya kihistoria ingawa historia peke yake haitoshi kuelezea uhalali wa Chama cha Mapinduzi kwa sasa kuongoza Taifa. TANu na ASP vilijijengea uhalali machoni mwa wananchi kwa kuwadhihirishia kuwa vinastahili kuongoza kutokana na usahihi wa siasa na mbinu zao katika mapambano dhidi ya ukoloni, kwa vitendo vya kujitoa

mhanga vya wanachama na viongozi wa vyama hivyo na kwa kudhihirisha kwa vitendo kuwa ndio watetezi halisi wa maslahi ya wananchi. Hatua za kimapinduzi zilizochukuliwa Zanzibar baada ya Mapinduzi Januari 12, 1964, na hatua za kimapinduzi zilizofuatia kuangazwa kwa Azimio la Arusha Februari 5, 1967 zilijenga uhalali mpya wa ASP na TANU katika misingi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

107. Pamoja na uhalali wa kihistoria, ambao ni uhalali wa kurithi, Chama cha Mapinduzi chenyewe lazima kijitengee uhalali wake katika hali ya mapambano ya sasa kwa kudhihiisha kwa vitendo kuwa ndicho mtetezi wa kuaminika wa maslahi ya wakulima NA WAFANYAKAZI NCHINI. Kwa kuwa kukubalika na kuamini kwa ASP na TANU kulijengwa kwa vitendo vya kimapinduzi vya uamininifu na ukweli kwa umma na kwa kujitolea mhanga kwa wanachama na viongozi wa TANU na ASP wakati huo, vivyo hivyo, uhalali wa uongozi wa CCM na kukubalika na kuaminiwa kake na umma kutategemea vitendo vya kimapinduzi vya uaminifu na ukweli kwa umma vya wanachama na hasa viongozi wa CCM katika haakati za kila siku za kujenga ujamaa viwandani siku za kujenga na mijini. Hii ndiyo njia ya pekee ya kukifanya Chama kiwe ndani ya umma na kiwe mwakilishi wa kweli na halali wa matumaini yao ya haki.

108. Serikali ndicho chombo kikuu cha utekelezaji wa siasa ya Chama. Chama kinaiongoza Serikali na vyombo vyake kwanza kabisa kwa kutoa shabaha na malengo, siasa (sera), maelekezo na maagizo ya mara kwa mara ambayo Serikali huyatafasiri katika mipango ya utekelezaji na sheria. Hii ina maana kuwa Chama ndicho kinachowajibika kuzungumzia na kuamua juu ya masuala mazito na makubwa ya nchi kabla hayajaelekezwa serikalini kwa uchanmbuzi na utekelezaji.

109. Serikali kwa maumbile yake ni chombo cha madaraka ya mabavu. Serikali ni sheria, ni majeshi, ni mahakama na ni jela. Kwa hiyo, hata katika hali yetu ya demokrasia na ujamaa, wakati wote ni muhimu kwa Chama na umma kuwa na hakika na anayekabidhiwa madaraka haya ya Serikali maana yakiangukia mikononi mwa mpinga mapinduzi madaaka hayo yanaweza kutumiwa dhidi ya maslahi ya umma wenyewe. Hivyo, kuhakikishanpia kuwa madaraka muhimu ya

Serikali na ya mashirika ya umma wanakabidhiwa watu ambao pamoja na uwezo wao wa kitaalamu ni wenye msimamo wa kizalendo na waaminifu kwa Chama na kwa wakulima na wafanyakazi wa Tanzania.

110. Kuhusu suala hili, Chama cha Mapinduzi kina kazi mbele yake ya kujumlisha tuliyojifunza tangu tupate uhuru na hasa baada ya Azimio la Arusha juu ya hatari zinazoweza kutokea kwa siasa ya Chama na kwa taifa wakati madaraka muhimu ya Chama, Serikali au Mashirika ya Umma wanakabidhiwa watu ambao kisiasa ni chui katika ngozi ya kondoo.

111. Serikali na Mashirika ya Umma vile vile ni vyombo vya kutoa huduma kwa wananchi. Katika nafasi yake ya uongozi, Chama kina wajibu wa kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma kwa umma hausababishi manung'uniko. Kuongoza katika hali hii maana yake ni kuwaelimisha na kuwasaidia watendaji katika siasa ili kuinua na kuimarisha ari na uwezo wao wa kutoa huduma. Wakati huo huo kuongoza ni kuwaelimisha na kuwaelekez wananchi juu a maamuzi halali ya serikali na umuhimu wa kuyatekeleza kwa maendeleo yao na ya taifa na pia wakati wote kuhakikisha kuwa wananchi hawafichwi au kudanganywa juu ya hali halisi na matatizo ya kweli ya nchi yao.

112. Aidha katika nafasi yake ya kiongozi wa serikali na vyombo vyake, Chama kina wajibu wa kuhakikisha kuwa muundo, taratibu na utendaji kazi wa serikali na wa mashirika ni wenye kutekeleza siasa ya Chama kama ilivyokusudiwa na kuleta ufanisi. Hapa ni muhimu kusisitiza kuwa Chama kiongoze mapambano dhidi ya umangi meza na tabia zozote zionazozorotesha kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma. Chama kione pia kuwa mifumo iliyopo Serikalini na katika Mashirika ya Umma inamwezesha mfanyakazi kushiriki katika uongozi wa kazi mahali alipo na kwamba kwa kushirikiana na wenzake anapata nafasi anayostahili ya kulijenga na kulitumikia Taifa lake.

**Chama na mfumo wa siasa na jamii**

113. Chama cha Mapinduzi ni muungano wa wakulima na Wafanyakazi wa mstari wa mbele kaika mapambano ya kujenga Ujmaa tanzania. Mfumo wetu wa kisiasa na kijamii unajengwa kwa mujibu wa msingi na mahitaji ya nchi inayojenga ujamaa. Lengo ni kujenga mfumo wa demokrasia ya kijamaa ambamo wakulima, wafanyakazi, washirika na atu wote wanaoishi kwa jasho lao sio tu kuwa watashirikiana na kuwa na kauli ya mwisho katika mambo ya siasa na ya jamii ya nchi yao bali wakati huo huo watamiliki na kudhibiti uchumi wa Taifa kwa kupitia Serikali, Mashirika ya umma, Vijiji vya ujamaa na vyama vya ushirika, Demokrasia ya Chama kimoja ya sasa ni hatua inayotuelekeza kwenye lengo hilo.

114. Hivyo ni muhimu kwa Chama katika kipindi kinachoanza sasa kuonyesha njia itakayolielekeza Taifa kwenye kiwango cha juu zaidi cha demokrasia ya wakulima na wafanyakazi washiriki kila hali inapohitaji ifanyike hivyo. Katika maana hiyo, ni muhimu kwa chama kuutazama tena mfumo wa demokrasia yetu ya Chama kimoja kwa lengo la kuuimarisha.

115. Kwanza kuna suala la mgawanyo wa madaraka ya nchi kati ya Chama, Rais wa Jamhuri ya Muungano na Bunge na kati ya Chama , Rais wa Zanzibar na Baraza la Wawakilishi. Sasa ni miaka ishiriki tangu Tanzania bara ipate uhuru na miaka 18 tangu Mapinduzi ya Zanzibar. Huu ni wakati unaofaa kutazama upya mfumo wa madaraka wa nchi yetu ili kuchukua hatua za kuimaisha uongozi wa pamoja kwa kutoa madaraka zaidi kwa Bunge ambalo pamoja na Rais ndio wawakilishi wa taifa. Kulipa Bunge madaraka zaidi ya kusimamia utekelezaji wa serikali ni kuimarisha madaraka ya Umma.

116. Jambo la pili ni kuwa bunge lenyewe linahitaji kufanyiwa uchambuzi kwa madhumuni ya kuimarisha uwakilishaji wa maslahi ya wakulima na wafanyakazi. Chama kitatumia kipindi kinachoanza sasa kutafakari juu ya njia bora zaidi zitakazohakikisha kuwa wakulima, wafanyakazi, washirika, vijana na wanawake wote wanwakilishwa kulingana na nia ya Chama ya kuendeleza mapinduzi yetu ambayo yanahitaji Bunge linalowakilisha maslahi halisi ya Wakuima na

Wafanyakazi na kwa kutia maanani nafasi ya wanawake na vijana katika Taifa letu.

117. Jambo ala tatu linahusu wabunge wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa. Bunge letu katika sura yake ya sasa lina asilimia kubwa ya wateuliwa. Chama kitalifafakari suala hili ili kuona kuwa ubunge wa kuchaguliwa unapata nafasi kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa ikieleweka kuwa uchaguzi wa wawakilishi ni sehemu muhimu ya demokrasia ya kijamaa.

118. Wakati huo huo, Chama kitafanya uchambuzi ili kupata njia za kuimarisha madaraka ya umma tangu vijijini hadi Taifa kwa jumla. Chama kitayarudia maamuzi yake ya nyuma kuhusu suala hili tangu tupata uhuru hadi sasa ili kujipa msingi wa kubuni utaratibu wa kujenga madaraka ya umma yatakayotuelekeza kwenye demokrasia ya kijamaa, katika jitihada hii, Chama kitaepuka jaribio la kurudisha mifumo ya tawala za kizamani, badala yake Chama kitajifunza toka mifumo ya zamani na hata ya nchi nyingine ili kubuni mfumo mpya utakaolingana na mahitaji ya maendeleo ya kidemokrasia na ya ujamaa ya tanzania ya leo na ya kesho. Hivyo, Chama kitayashughulikia masuala ya madaraka ya miji, wilaya na vijiji pamoja na suala la vyama vya ushirika katika msimamo huo.

119. Kwa hiyo, Chama pia kina wajibu wa kuhakikisha kuwa wananchi katika fani zote za maisha wanashiriki kwa ukamilifu katika ujenzi wa taifa lao. Katika nchi yetu wakulima na wafanyakazi ndio msingi wa mfumo wa jamii yetu na siasa ya ujamaa ya Chama ni siasa ya tabaka hili. Hivyo harakati za kujenga ujamaa ni harakati za kuwaendeleza wakulima na wafanyakazi. Pamoja na hayo, Chama kinatambua nafasi maalum ya wanawake na vijana katika mapambano yetu. Lengo hili linaweza kufikiwa kwa kupitia Jumuiya ya wafanyakazi, Jumuiya ya vijana, Jumuiya ya wanawake na Jumuiya ys Washirika. Suala la Jumuiya ni suala ambalo Chama kinahitaji likufanyia uchambuzi zaidi ili kufafanua waziwazi uhusiano wake na Chama na nafasi yao halisi katika harakati za ujenzi wa Taifa.

120. Pamoja na suala la Jumuiya za Wananchi kuna umuhimu kwa Chama kuunda mazingira nchini yatakayowawezesha wakulima na wafanyakazi kushiriki kwa ukamilifu zaidi katika mapambano ya kisiasa na ya kiitikadi. Miaka iliyofuata Azimio la Arusha na baadaye mwongozo wa TANU ilikuwa kipindi cha vuguvugu la kimapinduzi lililowawezesha vijana, wakulima na wafanyakazi nchini kushiriki katika kuijadili siasa ya Chama na kujiendeleza kinadharia na kiitikadi. Utekelezaji wa Mwongozo wa Chama cha mapinduzi unahitaji vuguvugu la namna yake. Hakuna msukumo wa kweli wa ujenzi wa ujamaa unaowezekana bila ya msukumo unaolingana na mijadala juu ya nadharia na itikadi ya ujamaa. Chama kitaunda mazingira nchini yatakayouwezesha umma kushiriki kwa nadharia na kwa vitendo katika utekelezaji wa maelekezo ya mwongozo wa Chama.

121. Tabia moja ya mapinduzi iliyoanza kujengeka wakati wa mwongozo wa TANI|U na imefifia sasasa na ile ya wafanyakazi na vijana wa nyuoni na shule za sekondari kujenga uhusiano wa kidugu na ushirikiano na vijiji vilivyo karibu nao. Maelfu ya wafanyakazi na vijana walifanya kazi za kujitolea wakati wa mwisho wa juma kudhihirisha mshikamano wa wakulima na wafanyakazi, na vijana katika kujenga ujamaa.

122. Utaratibu wa kazi za kujitolea kwa kwa wanachama wa Chama Cha Kijamaa, kwa wafanyakazi na vijana wana mapinduzi, ni jambo muhimu kwa maendeleo yao ya kisiasa na kiitikadi na kwa maendeleo ya ujamaa. Katika jitihada zake za kushirikisha umma katika ujenzi wa Taifa, Chama cha mapinduzi kitawajibika kufufua na kuendeleza tabia itakayowawezesha wana CCM, wafanyakazi na vijana kujitokeza kwa wingi katika kazi za kujitolea na kujenga ushirikiano kwa vitendo kwa vijana, wanajeshi, wakulima nawafanyakazi vijijini,

**Chama na siasa ya nchi za nje**

123. Siasa ya nchi za nje ya Chama cha Mapinduzi inaongozwa na misingi ya Uhuru wa taifa wa kujiamulia mambo yake bila kuingiliwa na yeyote; kushirikiana na vyama na nchi za kimaendeleo na za kijamaa katika kuimarisha mapambano

dhidi ya nguvu za ukoloni, ukoloni mamboleo, ubepari, ubeberu na ubaguzi wa rangi katika Afrika na kote duniani; kuunga mkono ukombozi wa Afrika na Umoja wa Afrika; na kushirikiana na mataifa mengine katika umoja wa nchi huru za Afrika, katika nchi zisizofungamana na upande wowote na katika Umoja w mataifa katika jitihada za kulinda na kudumisha amani na usalama duniani.

124. Kwa kuwa chimbuko la siasa yetu ya nje ni ya ndani ya ujamaa na kujitegemea tunayoijenga, basi kazi moja kubwa ya Chama na Serikali katika suala hili ni kuielezea siasa yetu na kutetea misingi ya haki, usawa na uhuru katika mikutano ya kimataifa na kulijengea Taifa uhusiano wa kidugu na ushirikiano na mataifa ya kimaendeleo na ya kimapinduzi na yale yot ambayo yanataka ushirikiano nasi katika misingi ya kuheshimiana, kutoingiliana katika mambo ya ndani na ya kuzingatia maslahi ya pande zote mbili.

125. Chama chetu, tangu wakati wa ASP na TANU kiliwajenga wanachama wake na wananchi kwa jumla katika hisia za kimapinduzi za kujishirikisha na mapambano ya ukombozi wa nchi nyingine za Asfrika na za dunia. Lakini pamoja na historia hiyo ya Chama na wananchi kushiriki kwa vitendo katika kuongoza siasa yetu ya nchi za nje, kumekuwa na vipindi ambapo shughuli za nchi za ne Chama kiliachia Serikali pekee.

126. Kuanzia sasa Chama kitahakikisha kuwa uhusiano wetu na nchi za kigeni unakuwa sehemu muhimu ya shughuli zake. Katika lengo hilo Chama kitaendeleza na kujenga uhusiano maalum na vyama halisi vya ukombozi, vya kijamaa na vya kimaendeleo vya Afrika na kote duniani ili kubadilishana uzoefu na kuimarisha mapambano dhidi ya ubeberu wa dunia.

## B CHAMA KUJIZATITI ILI KUONGOZA MAPINDUZI

*"Lakini Ujamaahauwezi kujijenga wenyewe. Kwani Ujamaa ni Imani. Hauna budi kujengwa na watu wanaoamini na kufuata kanuni zake. Mwana-TANU wa kweli ni mjamaa, wa wajamaa wenziwe yaani waamini wenziwe katika imani hii ya kisiasa na kiuchumi ni wote wale wanaopigania haki za wakulima na*

*wafanyakazi katika Afrika na popote duniani"*

**Azimio la Arusha**

127. Kazi kubwa ya Chama Cha Mapinduzi kwa mujibu wa Mwongozo huu ni kuchukua hatua za kujizatiti , kujijenga na kujiimarisha ilikujipa uwezo unaolingana na uzito wa mapambano hayliyo mbele yetu ya kujenga ujamaa katika kipindi ambapo ubepari na ubeberu wa dunia na vibwanyenye na wapinga ujamaa wa humuhumu nchini wanazidisha kujenga vitimbi vya uhasama dhidi ya siasa yetu ya ujamaa na Kujitegemea.

128. Kujizatiti kwa mapambano ya kujenga ujamaa kwanza kabisa ni kuwa na hakika na wapiganaji wa mstari wa mbele wa mapambano hayo ambao ni wanachama wa Chama Cha mapinduzi.. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ya Chama kujizatiti kwa wanachama wa CCM kifikra na vitendo, mmoja mmoja na katika umoja wao. Kutimiza wajibu wao wa kimapinduzi.

**Kazi ya kuwajenga na kuwaimarisha wanachama:**

*(a) Maandalizi: Vuguvugu la mijadala ya kichama katika Mashina, Matawi na Nchini kote.*

129. Chuo Kikuu cha Wanamapinduzi duniani kote ni kushiriki kwa vitendo katika harakati za kimapinduzi pale walipo. Chuo cha kuwajenga Wana CCM katika msimamo wa kimapinduzi pale walipo, kama ni kijijini, kiwandani, ofisini, jeshini, chuoni au katika kata ya mjini wanakoishi. Kushiriki kwa vitendo vya kujiendeleza au kujinoa katika nadharia ya mapinduzi.

130. Kwa hiyo, hatua ya kwanza kuelekea kwenye lengo litakalomwezesha mwana CCM kushiriki katika harakati za mapinduzi pale alipo ni kwa Chama kuanzisha mashina na matawi nchini kote. Mikutano hii ya wana CCM tu iitishwe kujadili maendeleo ya Chama katika sehemu zao; wanachama wakosoane na kujikosoa kuhusu vitendo vyao kama wanachama wakosoane na kujikosoa kuhusu vitendo

vyao kama wanachama ili kuona kama vinafafa na mahitaji ya mapinduzi. Mikutano hii pia izungumzie hali ya uchumi ilivyo nchini na kuchambua hatua za kujihami zinazotarajiwa kuchukuliwa na Taifa na katika sehemu zao.

131. Viongozi na maafisa wa Chama wa ngazi zote wawajibike kushiriki ktika mijadala hii kama wanachama wengine. Mijadala hii iwe na lengo la kumwezesha kila mwanachama na kila Tawi kudhihirisha walivyojitahidi kutekeleza majukumu yake katika chama, wapi mwanachama (tawi) alipoonyesha udhaifu na kutafuta njia za kutimiza majukumu vizuri zaidi.

132. Vuguvugu hili la mikutano ya wanachama liende sambama na mijadala ya hadhara ya wananchi wote vijijini, katika sehemu za kazi na mijini. Mikoa ipange mipango itakayowawezesha viongozi wa Chama wa ngazi zote kwenda vijijini, viwandani, majeshini, vyuongozi wa Chama wa ngazi zote kwenda vijijini, viwandani, majeshini, vyuoni na mijini kuelezea kwa kinaganaga hali ya uchumi wetu na hatua za kujihami kiuchumi ambazo lazima zichukulwe. Kushiriki huku kutawapa nafasi ya kujifunza na kuielewa zaidi hali ya nchi. Wakati huo huo magazeti na redio vitumike na Chama kuendeleza na kuelekeza mijadala hii.

133. Mijadala hii ya wanachama na ya wananchi kwa jumla itasaidia wananchi, kuelimisha zaidi juu ya matatizo ya nchi yetu na kuwaongezea ari ya kudhaminiria kushiriki kwa ukamilifu za zaidi katika harakati za kujihami kiuchumi na kisiasa. Mijadala hii katika Matawi, ikiendeshwa kwa makini na kwa utaratibu mzuri, itawezesha wanachama wa kweli kufahamiana na wanachama wa bandia kufichuliwa. Hii itahusu pia viongozi kueleweka katika msimamo.

134. Katika hali hii, hatua inayofuata ni kwa kila Tawi la Chama kuchukua hatua ya kuwajadili wanachama wake mmoja mmoja ili kuamua kama bado wanastahili kundelea na uanachama au la. Kwa kuwa wazembe, wazururaji, wezi na majambazi watakuwa wamefichuliwa katika vikao hivi, kwa kuwa wapinga ujamaa kiitikadi na kwa vitendo watakuwa pia wamefichukuliwa, basi hii ndiyo nafasi ya kukitakasa Chama. Matawi yapendekeze kwenye vikao vya juu hatua za kuwachulia wanachama watakaodhihirika kuwa hawatimizi masharti na wajibu

wa wanachama. Azimio la Arusha linasisitiza juu ya ubora wa wanachama badala ya wingi wa wanachama. Vuvuvugu hili la mijadala ya wanachama wenyewe tu litasaidia kuunda hali itakayowezesha kupiga hatua za mwanzo za kuelekea kwenye lengo hilo la Azimio la Arusha.

135. Kazi hii ya Chama ya kuongoza mijadla ya kujikosoa na kukosoana iendelee hadi itakapofikia kipindi cha mikutano mkiuu ya mwaka wa tano tangu CCM kuzaliwa. Kipindi hiki ni kirefu cha kutosha kwa mashina na matawi ya Chama kufanya vikao kadhaa vya wanachama wote ili kuwezesha kuelewana na kupimana kwa makini. Kipindi hiki ni kizuri pia kupimana kwa sababu ni kipindi ambapo Chama kitaongoza mapambano ya utekelezaji wa hatua za kujihami kiuchumi nchini kota. Na wakai huo huo hiki ni kipindi cha kuanzisha mksukumo mpya wa ujenzi wa ujamaa nchini.

136. Ni dhahiri kuwa katika hali hii ya vuguvugu la mapinduzi la utekelezji wa siasa ya Chama, wanachama matawini watapata nafasi nzuri ya kufahamiana na kuelewana kwa vitendo. Wana CCM halisi watajitokeza kwa vitendo katika utendaji wao wa kila siku kazini na wanakoishi. Wana CCM wa vijijini watadhihirisha uanachama wao kwa kuwa katika mstari wa mbele katika kutekeleza majukumu ya Ujamaa ya kijiji na katika kushiriki kwa dhati katika kazi za kujitolea kwa jumla kama ujenzi wa shule, zahanati, barabara za kijiji, shamba la kijiji, kushiriki katika elimu ya watu wazima, ulinzi wa kijiji na kadhalika.

137. Wana CCM wafanyakazi, watadhihirisha uanachama wao kwa vitendo kwa kufanya kazi kwa makini na kwa nidhamu, kwa kushirikiana na wafanyakazi wenzao kuhakikisha kuwa malengo ya kazi yaliyowekwa yanatimizwa, kwa kupambana bila woga na vitendo vyo vyote vile vya uvivu na ezembe kazini, vya kuzorotesha kazi au vya kuhujumu uchumi.

*(b) Mafunzo ya Siasa ya Chama*

138. Hama kinapanga na kuendesha mafunzo ya siasa yake ikiwa na malengo makubwa matatu: Mafunzo ya Siasa ya Chama yanatolewa kwa wananchi kwa

jumla kwa lengo la kuieneza siasa hiyo ili ieleweke na kukubalika na wakati huo ili kupiga vita upotoshaji na uzushi juu ya siasa ya ujamaa unaoenezwa na maadui wa ujamaa kwa nia ya kukifanya Chama kifarakane na Umma. Nia wakati wote ni kuelimisha umma na kuufanya uwe karibu zaidi na Chama ili ushiriki katika kutekelezas maelekezo na mwito wake kwa ari na hiari.

139. Lengo la pili la mafunzo ya siasa ya Chama ni kuhakikisha kuwa wananchi katika taasisi maalum za wananchi katika taasisi maalum za wananchi: wanafunzi, wanajeshi, wafanyakazi, vijana, wanawake, wanautamaduni, viongozi wa kazi, wandishi wa habari n,k, wanahamasishwa ili kuinua mwamko wao wa kisiasa, na kuwapa wahusika mwelekeo wa siasa kulingana na jinsi Chama kinavyoiona nafasi yao katika ujenzi wa taifa kwa sasa na kwa baadaye.

140. Lengo la tatu la mafunzo ya siasa ya Chama ni kuhakikisha kuwa wanachama na viongozi wanaimarika katika itikadi ya ujamaa na kujitegemea; kuwapanua wanachama na viongozi upeo wao wa kuyaelewa masuala mbalimbali; kuwapa methodolojia na mantiki ya kutafakari na kufanya uchambuzi wa msuala; kuwazatiti kwa hoja na mbinu zitakazowasaidia katika harakati za kuongoza utekelezaji wa siasa ya ujamaa pia kueneza na kutetea siasa ya Chama.

141. Mafunzo ya aina zote tatu ni muhimu kwa maendeleo ya mapinduzi yetu. Mafunzo ya aina ya tatu, yaani mafunzo ya wanachama na viongozi, ndiyo yatakayowezesha kufanikiwa kwa mafunzo ya aina ya kwanza na ya pili. Katika miaka ya usoni, Chama kitaendelea kuendesha mafunzo ya siasa ya Chama kwa mipango na msukumo mkubwa zaidi kwa kuzingatia kuwa mapambano ya kisiasa na kiitikadi ni sehemu muhimu ya mapambano ya kujenga ujamaa na kuzifichua na kuzishinda mbinu za adui.

142. Hivyo, Chama kitachukua hatua za kuimarisha na kupanua mipango ya mafunzo ya wanachama na viongozi. Wanachama walio wengi itabidi wapate mafunzo yao ya nadharia matawini kwao. Mafunzo hayo yatakayoendeshwa kwa msingi wa semina yatasimamiwa na mikoa na wilya zenyewe. Wanachama watakaojitokeza, kwa msimamo na uwezo, yaani wanachama wenye sifa za

kada, pamoja na viongozi wa matawi, wilaya, mikoa na Taifa wataingia katika mpango maalum wa kupata mafunzo katika vyuo vya Chama vya ngazi zinazolingana na mahitji yao. Utaratibu katika vyuo vya chama wa mafunzo ya kada na viongozi wa Chama utahitaji maandalizi ya makini na ya hali ya juu.

143. Chuo cha Chama ni mahala anapopelekwa katika chama, yaani kada wa Chama au kiongozi wa Chama, kwa madhumuni ya kumwandaa kwa kazi kubwa zaidi za Chama. Chama ndicho kinachomwandaa mwanachama mwenye msimamo wa sifa za kada wa Chama au kinaamua kumpeleka chuoni apate upeo mkubwa zaidi wa kukitumika Chama. Mwanachama huyu anaweza akawa afisa wa serikali, mfanyakazi wa chama au mkulima. La msingi ni kuwa anateuliwa na Chama kutokana na sifa zake katika Chama na kwa madhumun ya Chama na kwa madhumuni ya Chama ya kuendeleza kazi zake za kuongza Taifa kama Chama.

144. Wakati huo huo Chama kitaimarisha mafunzo ya siasa ya Chama ya aina ya pili kwa ajili ya taasisi kama majeshi, shule na vyuo, wafanyakazi, vijana pamoja na wataalamu na Wakuu wa kazi wa viwango na taasisi mbalimbali. Kwa utaratibu, mafunzo ya sina hii huendeshwa kwenye taasisi zenyewe na kusimamiwa na chama.

145. Mafunzo haya ya siasa ya Chama yatatumika pia kuwatambua wale wenye sifa za kada wa Chama. Wale watakaobinika kuwa wana welekeo huo basi wataingizwa katika utaratibu wa kupatiwa mafunzo zaidi katika vyuo vya Chama. Hii ina maana kuwa maafisa wa serikali na mashirika yake hata wafanyakazi katika sekta ya kibepari walio wana CCM wakijitokeza katika mafunzo ya Chama ya taasisi zao kwa KUWA WANA SIFA ZA KADA WA Chama watafanyiwa mpango ili inapotokea nafasi wajiunge na vyuo vya Chama.

## 2. Kuimarisha muundo, demokrasia na uendaji wa Chama:

146. Vyama hujipa muundo unaowesesha shughuli zake kutekelezwa kwa nidhamu na ufanisi. Kwa madhumuni hayo vyama hujipa vikao vya aina tatu hivi katika kila kiwango: Kikao cha aina ya Mkutano Mkuu ambacho ni cha wajumbe wengi na

ndicho kikao kinachotoa mwelekeo na kupanga siasa na mambo makubwa ya kutekelezwa katika kipindi kirefu kifuatacho. Vikao vya aina hii hukutana baada ya kipindi kirefu kupita. Kikao cha aina ya pili ni kipana na kina wajumbe wengi na ndicho kinachoongoza na kusimamia utekelezaji na maamuzi ya mkutano mkuu. Mwisho huwa kuna chombo kidogo cha wajumbe wachache ambao huunda Kamati ya utendaji ya kikao kikubwa cha aina ya pili.

147. Sasa, utaratibu wa zamani wa TANu na wa ASP ulikuwa na mfumo wa aina hii. Na uzoefu tulioupata hadi sasa unadhihirisha ubora wa mfumo wa aina hii maana unaunganisha mahitaji ya demokrasia pana ya vikao vya aina ya kwanza na ya pili na wakati huo huo unarahisisha utendaji kwa kuwa na kamati ya utendaji ya Wajumbe wachache watakaokabidhiwa majukumu ya utendaji siasa wa kila siku. Chama kitachukua hatua za kurekebisha muundo wake wa sasa ili kulifikia lengo hili katika ngazi zote za Chama.

148. Imedhihiri pia kuwa kuna umuhimu kwa sasa wa kuimarisha demokrasia ya Chama katika kiwango cha Taifa na baadaye katika viwango vya chini yake. Hali ilivyo kikatiba hivi sasa ni kuwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ni mchanganyiko wa wanaochaguliwa na wanaoteuliwa. Wakati umefika wa kuimarisha demokrasis ya Chama kwa kurekebisha Katiba ili wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa watokana na uchaguzi wa Chama.

149. Hatua nyingine inayohitaji kuchukuliwa ili kuimaisha Chama inahusu kuunganisha uongozi wa Chama yaani wa halmashauri Kuu ya Taifa na utendaji kazi wa Ofisi yake yaani Makao Makuu ya Chama. Mfumo wa hivi sasa una hitilafu inayoathiri kazi za Chama. Kwa mujibu wa mfumo huu viongozi kazi yao ni kuamua katika vikao na halafu kuna watendaji ambao ni maafisa waajiriwa wa Chama wa kutekeleza maamuzi hayo. Chama kitaurekebisdha utaratibu huu (pamoja na mfumo wa sasa wa Kamati za Kamati Kuu) kwa kuweka utendaji kazi za Halmashauri ya Taifa chini ya makatibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa yenyewe. Kazi muhimu za Halmashauri Kuu ya Taifa ni pamoja na Elimu. Uenezi na Itikadi ya Siasa, Uchumi na Mipango, Organaizesheni, Ulinzi na Usalama, Uhusiano na Nchi za Nje na Nidhamu na Udhibiti. Utaratibu huu utahusu Mikoa,

Wilaya na Matawi kwa hatua zitakazoamuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

**(3) Kuimarisha uongozi wa Chama katika sehemu zas kazi**

150. Kuanzia sasa Chama kitahakikisha kuwa serikali inachukua hatua za kuuwezesha utaratibu wa malengo ya utoaji maji kutumika katika viwanda na mashirika yake na kuinua uwezo wa utoaji huduma wa vyombo vyake. Wakakti huo huo Chama kitahakikisha kuwa wakuu wa kazi wanasaidia kisiasa ili wawe na msimamo wa kizalendo utakaoimarisha uwezo wao wa kitaalamu.

151. Hata hivyo, kazi kubwa ya Chama katika sehemu ya kazi itakafanywa na Tawi la Chama la mahali pa kazi panapohusika. Kazi ya Chama katika Taifa, Mkoa na Wilaya ni kuunda hali itakayoliwezesha Tawi la Chama kutekeleza wajibu wake wa uongozi. Ili kuhakikisha kuwa Chama katika sehemu ya kazi kinashika nafasi yake ya uongozi kuna masuala kadhaa ya kutia manani.

152. La kwanza ni kuwa suala la umuhimu wa kwanza kwa Chama katika mahali pa kazi katika mazingira ya nchi inayojenga ujamaa ni kuleta nmafanikio ya utekelezaji wa kazi. Hivyo, jitihada ya Chama katika sehemu ya kazi ni kuhakikisha kuwa wanachama na viongozi wa chama wanakuwa katika msitari wa mbele katika kutimiza wajibu wao wa kazi na kuona kuwa malengo yaliyowekwa yanafikiwa. Ni mwiko kwa mwanachama wa CCM au kiongozi kuwa miongoni mwa wategaji, wavivu na wazoroteshaji kazi.

153. Jambo la pili ni kuwa vyama vya kijamaa halisi haviongozi kwa mambavu bali kwa kuelimisha, kushawishi, kuelekeza na kwa chama chenyewe kuonyesha njia kwa vitendo. Kwa hiyo, kazi ya Chama katika sehemu za kazi itakuwa kuwajenga wana CCM kujua namna ya kuwashirikisha wafanyakazi wenzao katika kutekeleza malengo na wajibu wa kazi kutokana na mfano wao wenyewe wa kutekeleza wajibu kwa makini na kwa ari na uwezo wao wa kushawishi, kushauri na kuwashirikisha wafanyakazi.

154. Jambo la tatu la kuzingatia kuhusu suala la uongozi wa Chama katika sehemu za kazi ni kuwa "ujuzi ni madaraka." Watu wana tabia ya kumsikiliza anayejua zaidi kuliko wao juu ya suala fulani. Sasa. Mahali pa kazi ni malhali penye ujuzi wa aina mbalimbali. Atakayejitokeza kuwa anajua zidi katika fani fulani wenzake humheshimu, kumtegemea na kumsikiliza. Chama kitahakikishakuwa katika siku za usoni wanachama wa CCM wanajiendeleza katika fani zao za kazi ili kuwa miongoni mwa wanaotegemewa na kusikilizwa na wafanyakazi wenzao katika fani zao za kazi.

155. Jambo la nne linahusu matatizo ya kila siku ya wafanyakazi. Kiongozi, pamoja na sifa nyingine, ni mtu mwenye kuyaelewa matatizo ya watu na anayejua vile vile kuyaelezea na kuyajengea hoja. Chama kitahakikisha kuwa wanachama wa CCM kwanaaminiwa na wafanyakazi wenzao kwa kuwa wanayaelewa matatizo yao na wana uwezo wa kuyaelezea kwa ufasaha na kushirikiana nao katika kutafuta jawabu. Ili kufikia hapo ana CCM watawajibika kujiendeleza katika nadhari ya Chama na elimu kwa jumla.

156. Suala linarudia pale pale tulipoanzia. Kwa Chama cha mapinduzi kuongoza mapinduzi katika sehemu za kazi, kazi ya msingi ni kuwaandaa wanachama na viongozi wa matawini kwa mafunzo thabiti ya siasa ya Chama; ni kwa Chama kuhakikisha kuwa katika kila sehemu ya kazi viongozi wa Chama waliopo na wanachama kwa jumla wanapata miongoni mwao kada wa Chama wenye uwezo wa juu wa uchambuzi na mbinu watakaosaidiana nao katika mawimbi ya harakati. Hii ndiyo kazi kubwa ya Chama katika siku zijazo.

K.m. Katika jitihada za kuimarisha uongozi wa chama katika majeshi, miradi muhimu ya Taifa na taasisi, Chama kinaweza kuteua kamisaa wa siasa na kumpeleka katika sehemu hiyo. Kazi yake ni kusaidiana na uongozi uliopo kuimarisha utekelezaji wa majukumu, kuendeleza nidhamu na kwa kusaidiana na Chama katika sehemu hizi, kuuinua mwamko wa siasa na wa uzalendo wa wapiganaji, wafanyakazi au wanafunzi na kuwaongezea ari katika utekelezaji wao.

**Matawi na Mashina ya kazini na mijini kuimarishwa**

157. Ili Chama kitimize wajibu wake wa kuongoza katika sehemu za kazi tegemeo lake kubwa ni wanachama. Lakini wanachama pia wanategemea muundo wa mashina na matawi uliopo. Hivi sasa kuna matawi ambayo wanachama wao ni wengi mno kwamba uwezekano wao wa kufahamiana na kushirikiana ni mfinyu mno. Katgika siku zijazo Chama kitahakikisha kuwa katika sehemu za kazi suala la kuwaunganisha wanachama katika mashina linatiliwa mkazo zaidi. Wakati huo huo utatazamwa uwezekano wa kuunda matawi zaidi ya moja katika sehemu za kazi zenye wanachama wa CCM wengi mno.

158. Aidha, Chama kitalishughulikia suala la matawi ya Chama ya Kata zaMijini. Katika hali ya sasa matawi mengi ya kata za mjini ni makubwa kiasi kwamba wanachama hawawezi kujihusisha kwa ukamilifu katika matawi yao.

**(4) Kuimarisha Chama kwa kuimarisha uongozi**

159. Kiongozi wa Chama cha Mapinduzi kwamba kabisa lazima awe na msimamo wa kijamaa. Itikadi yake ya ujamaa, vitendo na tabia yake vijidhihirishe kwa wanaowaongoza, wanachama na wananchi, kuwa ni vya kijamaa. Imani ya kiongozi inaambukiza na kuimarisha imani ya anaowaongoza. Lakini kiongozi anayegunduliwa na anaowaongoza kuwa ni mnafiki kwa msimamo ni adui mkubwa kwa Chama maana anawavunja moyo wanachama, anawavuruga wananchi na kuunda hali itakayowafanya wananchi wasiwe na imani na viongozi wengine na Chama. Hivyo suala la viongozi wa Chama kuwa na msimamo sahihi kwa itikadi na katika maisha ya kila siku ni jambo lenye umuhimu wa kwanza kwa Chama cha Mapinduzi.

160. Lakini pia msimamo thabiti wa ujamaa wa kiongozi uambatane na uwezo wa kuongoza. Tumetamka hapo juu katika Mwongozo huu kuwa Chama cha Mapinduzi hakiongozi kwa mabavu bali kwa kuelimisha, kuelekeza, kushauri, kushawishi na kushirikiasha. Hii ina maana kuwa kiongozi wa Chama hana budi awe na uwezo wa kushauri na kuelimisha, kushawishi na kushirikisha, kwa jumla

awe na uweao wa kuieneza na kuitetea siasa ya Chama na kuwaunganisha wanadchama na wananchi katika harakati za kujenga ujamaa nchini na kwa kiwango cha uongozi wake.

161. Kutokana na hayo, Chama kuanzia sasa kitalipa uzito suala la msimamo na uwezo wa viongozi wake. Ndiyo kusema kwamba katika siku za usoni uchambuzi wa viongozi waliopo na waombao nafasi za uongozi utasisitiza juu ya msimamo wao kwa itikadi na kwa vitendo pamoja na uwezo wao wa kumudu uongozi huo.

162. Chama kitatumia njia mbali mbali za mafunzo ili kuwasaidia viongozi wenye nia njema kuimarisha msimamo wao kiitikadi. Chama pia kitakuwa na utaratibu wa kuwasaidia viongozi wenye msimamo sahihi lakini uwezo mdogo wa kuongoza kupata nafasi ya kuendeleza uwezo wao. Lakini Chama kitahakikisha kuwa viongozi ambao msimamo wao kwa itikadi na kwa vitendo ni kinyume cha misingi ya ujamaa hawapewi nafasi ya kukihujumu Chama kutoka ndani ya Chama. Wakati huo huo Chama kitahakikisha pia kuwa suala la uwezo linakuwa sehemu muhimu ya uchaguzi au uteuzi wa viongozi wa Chama cha Mapinduzi.

### (5) Maandalizi ya waombaji unachama

163. Chama kitaendelea kupokea wanachama wapya isipokuwa kwamba kuanzia sasa suala la wanachama litekeleze kwa vitendo agizo la Azimio la Arusha kuhusu ubora wa wanachama badala ya wingi wao. Wakati huo huo, jitihada zitafanywa ili kuhakikisha kuwa idadi ya wanachama wanawake, wakulima, wafanyakazi na vifaa inafanana na nafasi yao halisi katika jamii yetu.

*Mafunzo kwa waombaji uanachama:*

164. Mwelekeo na mkazo wa mafunzo ya wanachama wapya yatafanyiwa maadiliko ya kimsingi.

Mwanachama wa CCM kwa mujibu wa Mwongozo huu atapimwa kwa vitendo vyake vya kutekeleza siasa kwa vitendo vyake vya kutekeleza siasa ya Chama



57

katika maisha yake ya kila siku.  Vivyo hivyo, mtu anayeomba kuwa mwanachama wa CCM itabidi apewe kipindi cha majaribio ambapo atapimwa kuhusu kufaa kwake kuingia katka Chama kwanza kabisa kwa vitendo vyake v ya kutekeleza siasa ya Chama.  Aidha, atawajibika kuhusika na shina na tgawi ambalo ndilo litakalompangia majukumu ya kichama ya kuyatekeleza na ndiko atakakokuwa akijadiliwa hatua kwa hatua na uamuzi kufanywa kuhusu kuingizwa au kutoingizwa katika Chama wakati utakapofika.

**(6) Kuimarisha Chama kifedha**

165. Pamoja na kuimarisha usimamizi wa Fedha za Chama, Chaa kitachukua hatua thabiti za kujiimarisha kwa kujiongezea mapato mambo matatu yanakusudiwa kufanywa:-

Jambo la kwanza ni kuwa Chama kitaimarisha udhibiti wa fedha zake.  Jambo la pioi ni kuwa kitawataka wanachama na viongozi wa CCM kutoa mchango wa hiari wa kuimarisha Chama kwa kiwango cha asilimia itakayoamuliwa ya mshahara wa kila mwezi kwa kila kiongozi na mwanachama.  Utaratibu wa aina hiyo utabuniwa kwa ajili ya wachama wakulima na wanaojiajiri wenyewe.  Hatua ya tatu ni Chama kutafuta njia nyingine za kudumu za kukiwezesha kuongeza mapato yake.

**(7) Kuimarisha Jumuiya za Wananchi**

166. Jumuiya za wananchi zina umuhimu mkubwa sana kwa Chama katika malengo na mvinu zake za mapambano.  Pamoja na kuwa vyombo vinavyowaunganisha wananc hi wenye hali inayofanana katika shughuli zao za kazi za kila siku au wananchi wanaofanana kwa maumbile ili kuendeleza maslahi yao, Jumuia za wananchi pia ni mikondo inayokiwezesha Chama kuufikia umma wa wananchi kwa fikra, msimamo, maelekezo na miito mbali mbali.

167. Katika hali hii Jumuiya za wananchi zinaweza kuwa vyombo muhimu vya mapambano ya Chama na kuwa nguvu zake za akiba.  Katika kipihndi

kinachoanzia sasa, Chama kitajitahidi kuzijenga jumuia kwa kushirikiana nazo ili ziweze kuwa nguvu thabiti za mapinduzi ya kujenga ujamaa. Papo hapo, Chama kitahakikisha kuwa Jumuiya za wananchi zinapata msaada utakaoziwezesha kushirikiana na Chama bila ya kupoteza uwezo wao wa kuziendesha shughuli zao wenyewe bila ya kuingiliwa.

168. Kwa sasa, wakati Chama kinaanzisha vuguvugu la mapinduzi la mijadala ya kujikosa na kukosana kwenye Chama katika matawi yake, Jumuiya zichukue nafasi hii kushiriki kwa ukamilifu katika harakati hizi. Chama kitawataka wana CCM wote kuwa katika mstari wa mbele katika vuguvugu la kuleta mwamko wa siasa katika Jumuia zao. Ni wajibu kujiunga na Jumuiya zinazomhusu kueneza siasa ya Chama miongoni mwa wanachama wa Jumuiya hizo na kuwashawishi wananchi wengine kujiunga na Jumuiya.

**MWISHO**



59